**WAKULIMA** waoneshwa fursa masoko ya mazao nje

UKURASA 4



**WANAFUNZI** wasomea katika darasa lisilo na paa

UKURASA 10



**KAMALA** amkaba koo Trump Marekani

UKURASA 19


Wekezaji kurudisha miti asili nyenzo ayobadili maisha ya watu na vijiji
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe
CCM mnadeni kwa Kinana, mpeni kumbukumbu
Uzinduzi SGR mtaji unaomng'arisha Rais Samia nje, ndani ya mipaka
•Bwawa Mwalimu Nyerere bandari kumpaisha zaidi

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Agosti 2, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581756

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# NDOTO IMETIMIA

Usafiri SGR wazinduliwa baada ya miaka 29, Samia: ilikuwa vigumu...

Endelea Uk. 2



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akisafiri na abiria wengine kwa treni ya kisasa ya umeme (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, baada ya kuizindua rasmi katika eneo la Kilometa 0, Stesheni, jana. **PICHA: IKULU**

# Mbaroni madai kurusha pesa ovyo kwa kuwatunza maharusi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kurusha fedha ovyo sakafuni wakati wakimtunza bwana harusi na bibi harusi katika sherehe iliyokuwa ikifanyika katika moja ya kumbi za starehe jijini hapa.



Akithibitisha kukamatwa kwa watu hao, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Wilbroad Mutafungwa, alisema watuhumiwa hao walitenda kosa hilo Julai 7, mwaka huu, katika moja ya ukumbi wilayani Il-

ENDELEA UK 3

## Biteko akoleza moto wa uchaguzi Rais TLS

UKURASA 3

**MICHEZO** WACHEZAJI SIMBA WATOA AHADI NZITO UK 24

MAONI, KATUNI UK.6

# Ndoto yatimia SGR baada ya miaka 29

**Na Waandishi Wetu**

NDOTO imetimia. Ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan jana kuzindua usafiri wa treni ya kisasa ya reli kiwango cha kimataifa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma. Ni ndoto iliyoanza tangu serikali ya awamu ya tatu chini ya Rais Benjamin Mkapa na kutimia awamu ya sita.

Wazo la kuwapo kwa reli hiyo liliibuliwa na Mkapa baada ya kufanya mazungumzo na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, juu ya kujenga reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Kigali nchini Rwanda. Tangu kuwapo kwa wazo hilo, hivi sasa ni takriban miaka 29.

Ujenzi wa reli hiyo kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro yenye urefu wa kilomita 300 ulianza rasmi Aprili, 2017 katika uongozi wa Rais wa awamu ya tano, Hayati John Magufuli.

Alipoingia madarakani Machi 2021, Rais Samia alipokea kijiti cha ujenzi wa reli hiyo ikiwa imejengwa kwa urefu wa kilometa 722. Hadi jana ujenzi huo ulikuwa umefikia kilometa 1,522 kwa viwango tofauti tofauti.

Juni 14, mwaka huu, safari ya kwanza ya treni ya SGR ilianza toka Dar es Salaam hadi Morogoro ikiwa na mabehewa 14 na takribani abiria 700. Safari ya Dar es Salaam hadi Dodoma ilianza Julai 25, mwaka huu, kwa mabehewa 14 yenye jumla ya abiria 1,000.

Akiwa njiani kwenda Dodoma kwa ajili ya kuzindua treni hiyo jana, Rais Samia alisema anajisikia faraja kuona miradi aliyoianza kuitekeleza tangu awamu ya tano ikiwamo Daraja la Tanzanite, Bwawa la Umeme la Nyerere na SGR kuwa inakamilika na kuwahudumia wananchi.

Alisema anajisikia fahari kuwa licha ya mradi huo kuwa na ugumu katika utekelezaji wake lakini imefikia hatua ya kuzinduliwa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.

Rais Samia alisema isingekuwa rahisi kuiacha miradi hiyo kwa sababu ni muhimu sana katika kuwaletea wananchi maendeleo na kuchochea mendeleo endelevu.

"Kwenye serikali ya utawala bora na inayozungumzia maendeleo endelevu, huwezi kuiacha hiyo miradi. Hiyo miradi ni muhimu sana. Kila mmoja una umuhimu wake, nikasema naendelea na hii miradi," alisema.

Alisema hategemei mradi huo kuanza kutoa faida kwa sasa bali anauchukulia kama sehemu ya kutoa huduma kwa jamii na kuiletea maendeleo makubwa kupitia usafiri na usafirishaji kama ilivyo kwenye usafiri wa ndege.

Akiwa stesheni ya Pugu, alisema ujenzi wa reli hiyo unaendelea hadi Kigoma na mpaka wa Burundi na Jamhuri ya Congo, ili kupanua biashara za kimataifa na kuchochea maendeleo.

Rais alisema alisukumwa kutekeleza mradi huo uliogharimu takribani Sh. trilioni 10 na kuiunganisha nchi na mataifa jirani ikiwamo Demokrasia ya Congo ili kufungua fursa za biashara.

Alisema uwapo wa reli hiyo pia unachochea kukua kwa utalii kwa sababu sasa hivi watalii wanaokwenda Mikumi hawapandi tena ndege bali wanapanda treni mpaka Morogoro.



Treni hiyo, alisema licha ya kubeba abiria pia itatumika kusafirisha mizigo ya kibiashara kama vile mafuta tofauti na awali yalipokuwa yakisafirishwa na malori.

Alisema moja ya hasara za uwapo wa usafiri huo kupungua kwa magari barabarani katika miji ambayo treni inapita na kuwaathiri wafanyabisahara lakini akasema ni jambo jema kwa sababu itapunguza ajali za barabarani.

Rais alimwagiza Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, na mawaziri wengine kuhakikisha kuwa fedha zinazokusanywa kupitia kodi mbalimbali na kuingia katika akaunti za serikali, zinatumika kuondoa kero za wananchi zikiwamo umeme, maji na elimu.

Katika stesheni ya Kihonda mjini Morogoro, Rais aliwaahidi wananchi wa eneo hilo kuwa changamoto ya barabara inafanyiwa kazi kwa kuwa mkandarasi ameshapatikana. Aliwasihi wananchi wa mkoa wa Morogoro kutumia fursa ya uwapo wa treni hiyo kujinufaisha kiuchumi.

Rais Samia aliwataka Watanzania kutumia fursa ya treni ya kisasa iliyoanza kwa kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo zinakazowaingizia mapato kupitia masoko ya ndani na nje.

Alisema Watanzania wanapaswa kuongeza nguvu ya uwekezaji kwenye kilimo na shughuli zingine ili kukuza biashara kwa kutumia usafiri wa treni.

### WAMILIKI MABASI

Rais aliwashauri wamiliki wa mabasi kuendelea kutoa huduma katika maeneo mbalimbali ya nchi ambayo huduma za reli hazipatikani kutokana na mwingiliano wa uwekezaji mmoja na mwingine.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema tangu treni hiyo ianze safari Juni 25 hadi kufikia Julai 28, mwaka huu, wamesafirisha abiria 188,000 na takribani watu 7,000 kwa siku.

Kadogosa alisema treni hiyo pia inatumiwa na wasafiri wa mikoa ya mbali kama vile Mwanza kupunguza muda wa safari ambao wangetumia kama wangepanda mabasi ya kawaida.

"Wanapofika Dodoma wanapanda mabasi ya kwenda Mwanza, Iringa, Arusha, Kagera na mikoa mingine. Kwa hiyo mtu akitoka saa 12:00 asubuhi, anafika Dodoma na kuchukua basi saa 4:00 na anafika Mwanza saa 11:00 au 12:00 jioni wakati awali walikuwa wanafika saa 8:00 usiku," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuitumia Morogoro kama ushahidi wa mafanikio makubwa ya SGR na mkoa umekuwa kitovu cha SGR kwa kuwa na njia tano za kubadilisha treni tofauti na maeneo mengine.

Mbunge wa Morogoro Mjini (CCM), AbdulAziz Abood, alisema reli hiyo imeleta manufaa makubwa kwa wananchi kwa kuongeza uchumi kwa uwekezaji wa aina mbalimbali.

Naye mmoja wa wananchi, Julius Masini, aliishukuru serikali kwa hatua kubwa iliyopigwa inayoonesha kuleta fursa mbalimbali za maendeleo kijamii.

### MAJINA YA STESHENI

Akizindua rasmi usafiri wa treni ya SGR, Rais Samia alitoa majina ya stesheni za reli kwamba Dar es Salaam itaitwa John Magufuli, Jakaya Kikwete (Morogoro) , Samia (Dodoma) ,Tabora itaitwa Ali Hassan Mwinyi na Shinyanga itajulikana kama Abeid Amani Karume. Mwanza itaitwa Julius Nyerere na Kigoma Benjamin Mkapa.

Aidha, Rais Samia alisema Watanzania hawana budi kutambua na kupongeza jitihada za watangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli.

Alisema Desemba, mwaka jana, alitoa maagizo ya mradi huo kipande cha Dar es Saalam hadi Dodoma kianze kutoa huduma ifikapo Julai, mwaka huu, na hatimaye huduma zimeanza.

"Nilitoa maagizo haya baada ya kuona tarehe zinabadilika kila mara, hivyo niipongeze Wizara ya Uchukuzi na TRC kukamilisha kwa muda nilioagiza. Nitahakikisha miradi yote ya kimkakati ambayo iliachwa katika uongozi wa awamu ya tano inakamilika kwa wakati na kwa ubora zaidi," alisema.

Rais Samia pia alimwagiza Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, kukaa na TRC ili kuweka vigezo vya kazi na kuwezesha mradi huo kujiendesha kwa faida huku akiiagiza bodi ya wakurugenzi na menejimenti ya TRC kuhakikisha vipande vyote vya reli vilivyobaki vinakamilika kwa wakati.

"Wekeni mifumo ya kisasa ya uendeshaji wa reli hii. Sitegemei kuona TRC inaomba ruzuku ya serikali bali yenyewe ndiyo itakuwa inatoa gawio kwa serikali. Msajili wa hazina lisimamie hili," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alimpongeza Rais Samia kwa kufanikisha kukamilika kwa mradi huo ambao ulianza katika uongozi wa serikali ya awamu ya tano chini ya hayati Rais John Magufuli.

Alisema ujenzi wa mradi huo hadi sasa umetumia zaidi ya Sh. Trilioni 25 kwa kujenga kilometa 722 za reli na majengo 12 ya stesheni kubwa na ndogo na vituo vya kupozea umeme pamoja na miundombinu mingine

**Imeandikwa na Jenifer Gilla (DAR), Christina Haule (MOROGORO) na Paul Mabeja (DODOMA).**


**SUMAJKT AUCTION MART COMPANY LIMITED**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na CRDB BANK PLC, P.o.Box 268, 11101 Dar es Salaam, tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kulipa deni pamoja na gharama ya dalali. Iwapo watashindwa kufanya hivyo dhamana zao zitauzwa kwa mnada wa hadhara kwa mujibu wa mikataba husika kama inavyoonesha kwenye jedwali hapo chini, Mnada utafanyika dhamana ilipo.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA ILIPO | TAREHE NA MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | JEREMIA ENEZA MSUYA | NYUMBA ILIYOPO KWEMBE KING'AZI 'A' , WILAYA YA UBUNGO - DAR ES SALAAM | 23/08/2024 SAA 5:00 ASUBUHI |
| 2 | MARTHA KASENDILE MWAIPAJA | NYUMBA ILIYOPO ITUHA -ILOMBA, MBEYA | 27/08/2024 SAA 5:00 ASUBUHI |
| 3 | HILDA LUCAS NDAGA | NYUMBA ILIYOPO ITUHA - ILOMBA , MBEYA | 27/08/2024 SAA 8:00 MCHANA |
| 4 | CLAUDE PETER FUNGO | NYUMBA ILIYOPO MBUGANI, KYELA-MBEYA | 30/08/2024 SAA 5:00 ASUBUHI |
| 5 | LUCAS JOSEPH NGOMBO | NYUMBA / KIWANJA NA.370, KITALU 'MIKUMI', KYELA-MBEYA | 30/08/2024 SAA 8:00 MCHANA |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Nyumba itauzwa mahali ilipo na kama ilivyo.
2. Mteja anatakiwa kulipa 25% siku ya mnada na 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada.
   Endapo mteja atashindwa kumalizia 75% ndani ya siku 14 hatorudishiwa kiasi alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa
3. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
4. Nyumba itauzwa mahali ilipo na kama ilivyo.

**Kwa mawasiliano zaidi:-**
**0753063481/0758040099**
**auctionmart@sumajkt.go.tz**

HABARI KITAIFA

# Mbaroni madai kurusha pesa ovyo kwa kutunza maharusi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kurusha fedha ovyo sakafuni wakati wakimtunza bwana harusi na bibi harusi katika sherehe iliyokuwa ikifanyika katika moja ya kumbi za starehe jijini hapa.

Akithibitisha kukamatwa kwa watu hao, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Wilbroad Mutafungwa, alisema watuhumiwa hao walitenda kosa hilo Julai 7, mwaka huu, katika moja ya ukumbi wilayani Ilemela wakati wa sherehe ya Robert Shija.

Alitaja watuhumiwa hao kuwa ni Majani Mabele (47), mfanyabiashara na mkazi wa Nyansaka, Kiruma Lucas (31), mfanyabiashara na mkazi wa Ibanda, Sharifu Dotto (29), mfanyabiashara na mkazi wa Kiseke na Seleman Mbuga (39), mfanyabiashara na mkazi wa Nyamanoro wilayani Ilemela.

"Wote hao walionekana katika kipande cha video kilichokuwa kimerushwa mitandaoni wakitupa chini noti za fedha ya Kitanzania za Sh.10,000 na Dola za Kimarekani, huku wengine wakizizoa kutoka sakafuni kama uchafu," alibainisha DCP Mutafungwa.

Alisema kitendo cha wageni waalikwa katika sherehe mbalimbali urusha fedha chini wakati wa kutoa zawadi, wengine kuziokota na kuziweka kwenye kikapu kinaonesha taswira mbaya katika suala la utunzaji wa fedha za Kitanzania ambazo ni Tunu ya Taifa.

Aidha, aliwataka wakazi Mkoa wa Mwanza, kuzingatia utunzaji wa fedha ikiwa ni pamoja na kuacha kuchafua fedha makusudi kwa kuzikanyaga, kuzichana, kuzichora, kuzikusanya,kuzihifadhi kama uchafu na kuzikunja kitendo ambacho alikiita kuwa kinafifisha uhai wa fedha.

Hivi karibuni, Meneja Idara ya Uendeshaji Tawi la Dodoma wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Nalasco Maluli iliwaonya wananchi wanaorusha fedha sakafuni kwenye harusi, kuhifadhi fedha kwenye matiti, soksi, chini ya magunia na kufunga fundo kwenye kanga kwamba wanaifedhehesha fedha ya Tanzania.

Kadhalika, alisema vitendo hivyo ni kosa la jinai na atakayebainika atachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema watafikishwa mahakamani kwa kuwa noti na sarafu ni sehemu ya nyara za serikali ambazo zinapaswa kuthaminiwa.



Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji ambaye pia ni Mwakilishi wa Tanzania Umoja wa Ulaya, Jestas Nyamanga (kushoto), akizungumzia fursa mbalimbali zinazopatikana kati ya Tanzania, Ubelgiji na Umoja wa Ulaya, wakati wa kipindi cha Kumepambazuka katika Studio za Redio One, Mikocheni Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Biteko akoleza moto uchaguzi TLS

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko amewataka wanachama wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kuwachagua viongozi wanaotaka kusukuma haki na amani ya Tanzania, watakaowaunganisha badala ya kuwagawanya.

Pia, watakaoiweka taaluma yao kuwa ya heshima kwa jamii badala ya kujitafutia umaarufu.

Akifungua Mkutano Mkuu wa TLS, jijini Dodoma jana, ambao pamoja na mambo mengine utachagua viongozi wa chama hicho akiwamo rais na makamu wake.

"Inawezekana namna anavyozungumza hakufurahishi, au anatokea mahali ambako wewe hautokei, lakini kama ajenda yake ni kuufanya uwakili kuwa jambo la heshima kwenye jamii yetu na sio yeye binafsi kuwa maarufu, huyo, mfikirieni, mahali penye kuvumiliana pana maendeleo," alisema Dk. Biteko. Aliwataka watakaochaguliwa kufanya kazi ya kuwaunganisha na watakaoshindwa kuwaunga mkono watakaoshinda.

"Hicho ndicho kinatufanya tuwe wanadamu, tofauti zetu, lakini uwapo wenu kuna kitu kimoja kinawaunganisha, chenyewe hakiangalii tofauti hizo, ambacho ni taaluma na uanasheria wenu, kama atatokea mtu anaumizwa zaidi na uwakili wenu na angetamani unakuwa na maana kwa jamii ya Watanzania kwa ajili ya kusukuma haki na amani, ningekuwa mpiga kura ningesema huyo mwangalieni," alisema Dk. Biteko.

Alitoa wito kwa chama hicho, kuendelea kuwa na msisitizo kwa wanataaluma kukaa kwenye taaluma yao kama wanasheria na kuwa na kiu ya kuendeleza chama chao.

"Mwendelee kuwa na kiu ya kuona chama chenu kinakua zaidi na kinaendelea kutekeleza majukumu yake kwa manufaa ya Watanzania wote. Nataka niwape siri moja wakati mnachaguana. Haiwezekani ndugu rais ukawa na chama cha watu wote hawa wasiwe na kabila, dini, wasiwe na mapenzi na timu ya mpira.

"Wamo wa timu nyingine, na wengine wana timu hii, au wana vyama vya siasa au ukanda wanakotokea, wameumbwa na Mungu, mvumiliane," alisema Dk. Biteko.

Aliwaomba wanataaluma wa TLS, kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuchagua viongozi wanaofaa ambao watawasaidia kutatua kero zao katika kipindi cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Tumieni mitandao yenu kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa uchaguzi huu na kwamba utakapofanyika uwe huru wa kila chama kunadi sera zake na kujenga mshikamano baina ya Watanzania na mkifanya kazi hiyo mtakuwa mmetusaidia kama serikali na kama taifa kupata viongozi wazuri, waliochaguliwa kwa sifa na si kwa sababu zozote ambazo haziwezi kutupa viongozi wazuri," alisema Dk. Biteko.

Kuhusu malalamiko ya TLS yaliyotolewa na rais anayemaliza muda wake, Harold Sungusia ya mawakili wao kukamatwa wanapotekeleza majukumu yao, Dk. Biteko alimwagiza Waziri wa Katiba na Sheria, Pindi Chana kushughulikia na kutatua kero hiyo.

"Rais wa TLS ameeleza kwamba kuna wakati wanakutana na changamoto wakati wa kutekeleza majukumu yao ikiwamo kukamatwa kwa mawakili. Waziri amelisikia, nchi hii inaendeshwa kwa utawala wa sheria, imani yangu ni kwamba pamoja na kulisikia na kulichukua, tutakapokutana mwakani hili lisiwe changamoto ya kulisema sana, tuwe tumelitafutia majibu," alisema Dk. Biteko. Kuhusu TLS kucheleweshwa kupewa miswada mbalimbali kwa ajili ya kuichambua na kutoa maoni yao, Dk.Biteko aliagiza wizara husika kulifanyia kazi.

"Unaweza ukatoa maoni yako kwa kurasa 45 na yasichukuliwe, muhimu ni umetoa maoni kama maoni ya TLS au ya mtu yeyote yamechukuliwa au hayajachukuliwa, muhimu ni kwamba kuna maoni ya wengine yamechukuliwa kwenye mswada huo.

"Kama ambavyo tunaweza kuchukua ya TLS, tukaacha ya mwingine, haimaanishi kwamba yamepuuzwa, ila inamaanisha 'engagement', kwamba kila jambo litakaloletwa kwa ajili ya kutoa maoni ya wajumbe hasa wa TLS kwa sababu ndio wanaoshughulika na sheria hizi kila wakati, tuchukue muda wa kutosha, kuzisoma na kuzisikiliza," alisema Dk. Biteko.

Rais wa chama hicho, Sungusia alishukuru serikali kwa kufanya maboresho ya sheria ya mawakili sura namba 341 na kuongeza kifungu cha 41 na 42 ambavyo vimeongeza ukali wa kushughulikia 'vishoka'.

"Nishukuru serikali mwaka jana ilibadilisha Sheria ya Mawakili sura namba 341 iliyorekebishwa mwaka jana, imeongeza ukali kwa vishoka na kuondoa kifungu cha miezi 12 na sasa ni miaka mitatu ikiwa kuna mtu atajifanya yeye ni wakili au atafanya kazi za uwakili wakati haruhusiwi," alisema Sungusia.

"Pamoja na faini ambayo imeongezwa kutoka Sh. 2000 mpaka Sh. milioni 20, kwa hiyo tunaona kuna mabadiliko makubwa na tunaamini kwamba tukiisimamia hii sheria tutapambana na wale watu wasiokuwa na maadili wanaowadanganya na kuwalaghai wananchi kwamba wao ni mawakili kumbe sio."

Pia, alisema chama hicho kimekuwa kikitoa elimu kwa wananchi inayohusu upatikanaji wa Katiba mpya na TLS inaona kuna haja ya kuwa na mjadala mpana wa kitaifa wa kujua ni namna taifa linaweza kusonga mbele katika kuendeleza elimu ya Katiba katika kuelekea kupatikana kwake.

## Wachimbaji waonywa utoroshaji wa madini

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

SHIRIKISHO la Wachimbaji Wadogo wa Madini Tanzania (FEMATA), limewaonya wachimbaji wanaokwepa kulipa mapato ya serikali na kujihusisha na utoroshaji wa madini kwa njia za magendo kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Onyo hilo lilitolewa jana na Rais wa FEMATA, John Bina, wakati akizungumza na wachimbaji wadogo mkoani Iringa na kusisitiza kuwa hawatakubali kuona madini yakisafirishwa kwa njia isiyo halali na kusababisha serikali kupoteza mapato.

"Kama kiongozi wa sekta hii, sitaki kuona makosa kabisa. Kabla serikali haijakushughulikia tutaanza sisi kukushughulikia. Utoroshaji wa madini haufai na haukubaliki, msituchafulie," alisema Bina.

Alisema kwa sasa asilimia 20 ya dhahabu inayopatikana nchini itanunuliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT),huku asilimia 80 ya dhahabu ikiuzwa kwenye masoko yaliyotengwa na serikali.

"Sasa hivi tumeshawaambia BoT wanataka kununua dhahabu ili tuwe na akiba ya kitaifa na sisi wachimbaji wadogo niwaambieni tumekubaliana kwamba BoT sasa wanunue dhahabu asilimia 20 kutoka kwa wachimbaji wadogo. Walikuja na ratiba ya kununua dhahabu yote tukawaambia hapana," alisema.

Bina aliwataka wachimbaji kuhakikisha wananunua vitambulisho vinavyotolewa na serikali, ili waweze kutambuliwa kirahisi na taasisi za kifedha pamoja na halmashauri mbalimbali nchini ili kupewa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na serikali kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu itakayowasaidia kuendesha shughuli zao.

Akiwasilisha taarifa kwa niaba ya wachimbaji wadogo mkoani Iringa, Ibrahim Msigwa ambaye pia ni mchimbaji mdogo wa madini mkoani hapa alisema wanakabiliwa na changamoto ya uchimbaji duni wa madini kutokana na mkoa kukosa utafiti wa kina.

Alisema Iringa ina madini ya kutosha lakini utafiti haukuwahi kufanyika hali inayosababisha wachimbaji wadogo kuchimba kwenye maeneo yasiyofanyiwa utafiti.

Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Iringa, Abdulrahman Milandu, alisema kwa sasa mkoa wa Iringa umeanza kupiga hatua katika ukuaji wa sekta hiyo ambayo ilikuwa ikisuasua kwa muda mrefu.

Alisema awali mchango wa sekta hiyo kwenye mapato ulikuwa hauzidi Sh. milioni 10 kwa mwaka lakini sasa kwenye kapu la makusanyo ya mapato ya madini, Iringa inakusanya Sh. bilioni moja na Sh. milioni mia mbili kwa mwaka.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA MAFUNZO YA UDEREVA CHINI YA MPANGO WA MAFUNZO WA EACOP KUMBUKUMBU NA: 00000556

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") linakaribisha makampuni yenye uzoefu na weledi kuonesha nia ya kutoa Huduma za Mafunzo ya Udereva chini ya Mpango wa Mafunzo wa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha mafuta chini ya ardhi na linalovuka mipaka ya nchi mbili ili kusafirisha mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale, Wilaya ya Hoima nchini Uganda hadi kwenye rasi ya Chongoleani, mkoani Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,443, kati ya hizo kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania na kilomita 296 zitakuwa chini Uganda.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

Chini ya mpango wa mafunzo EACOP, inalenga kuwawezesha vijana wa Kitanzania kufanya kazi wakiwa sehemu ya Uendeshaji wa EACOP kwa siku za baadaye. Programu hii ya mafunzo itashirikisha Watanzania wapatao 113. Moja ya lengo la mafunzo haya ni kuhakikisha wanafunzi wanapata leseni halali ya udereva kwa kuwa watahitajika kuendesha magari wakati wa programu ya mafunzo, na wakati wa uzinduzi na uendeshaji wa Mradi wa EACOP.

Hivyo basi, EACOP inahitaji mtoa huduma wa mafunzo ya udereva mwenye sifa na aliyethibitishwa na mamlaka husika, ili kutoa huduma hiyo kwa washiriki wa mafunzo wa EACOP ambao watakuwa katika vituo vya mafunzo vilivyopo katika mkoa wa **Arusha** na **Moshi**. Lengo kuu la mafunzo ya udereva litakuwa.

- Kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa udereva wa EACOP wapatao 100.
- Kuendesha mafunzo ya kupiga msasa maarifa ya udereva kwa idadi ya wanafunzi wa EACOP 113.
- Kuwa na idadi ya wanafunzi wahitimu wapatao 100 waliotunukiwa leseni halali za udereva za Tanzania.

Mafunzo ya udereva yatatolewa mkoani Arusha, kati ya mwezi Agosti 2024 na Oktoba 2024, yakifuatiwa na mafunzo hayo hayo yatakayofanyika mkoani Moshi, kati ya mwezi Novemba 2024 na Machi 2025. Baada ya kukamilika kwa mafunzo hayo hapo juu, kutafanyika mafunzo ya kupiga msasa madeva dereva 113 kuhusu mbinu za Udereva wa kujikinga yatakayofanyika mkoani Moshi kati ya mwezi Januari 2025 hadi Machi 2025. Matokeo ya mafunzo hayapaswi kupata leseni ya udereva pekee, bali pia kuwafundisha wanafunzi kufuata sheria na kanuni za barabarani, kuendesha gari kwa kujilinda, kudumisha mtazamo sahihi na kuboresha mbinu za udereva kwa usalama.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zinatakiwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatavyo:

- Vyeti vya Usajili vya Tanzania ukijumuisha cheti cha usajili, leseni ya biashara n.k.
- Uzoefu, utendaji na uwezo katika kutoa Huduma iliyoainishwa hapo juu kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania na uzoefu/utendaji wa kimataifa wa angalau miaka 10 ya utoaji wa huduma zinazofanana na hii kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Utendaji vya Shirika la fedha la Kimataifa IFC).
- Wasifu wa watendaji wakuu watakaohusika katika utoaji wa Huduma ikiwa ni pamoja na vyeti vyao, kiwango cha uhitimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika katika miradi mikuu ya mafuta na gesi.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka huu.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha kwa miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamejisajili au wametuma maombi ya kujisajili na kuthibitishwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kukidhi Kanuni za Tanzania za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017, pamoja na tafsiri ya Kampuni za Wazawa.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na usimamizi wa Haki za Binandamu.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu yanakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb). Maombi yatumwe kabla au mnamo tarehe 16 August 2024 saa **11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe: **00000556 - Utoaji wa huduma za Mafunzo ya Udereva.** Maombi yote ya kuonesha nia yasipungue au kuzidi kurasa 10 hadi 20. **Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiingereza.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

# Wakulima waoneshwa fursa soko la mazao nje

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka wakulima wa mazao ya chakula na matunda, kuongeza jitihada katika kilimo kwa kuwa kuna soko la uhakika nje ya nchi.

Majaliwa alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa Maonyesho ya 31 ya Nane Nane kitaifa yanayoendelea katika Uwanja wa Nzuguni, jijini Dodoma.

Akitoa mfano wa soko la mahindi, Waziri Mkuu alisema nchi ya DRC Congo wanahitaji tani 500,000 huku Zambia nayo ikieleza kuhitaji kiasi kikubwa cha nafaka na kwamba zipo nchi nyingine pia zinahitaji.

Alisema nchi za India, Brazil na Marekani kuna soko la matunda, pilipili hoho na mazao mengine ambayo uhakika wa soko upo.

"Hii ni fursa ambayo wakulima wanapaswa kuichangamkia kwa sababu serikali yao inapambana kutafuta masoko kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo wanachofanya," alisema Majaliwa.

Aidha, alisema Shirika la Chakula Duniani (FAO), lina uhitaji wa mahindi, kilichopo ni wakulima kuchangamkia fursa hiyo, ili waweze kuinuka kiuchumi pia kupanua wigo wa kilimo wanachofanya.

Alisema ni vyema wakulima wakatumia fursa ya Maonyesho ya Nane Nane Kitaifa Dodoma, kujiinua kiuchumi ili waweze kupiga hatua katika biashara zao. Alisema pia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), kuendelea kukusanya chakula kwa kuwa hatua hiyo itaongeza soko la uhakika wa mazao ya wakulima na upatikanaji wa chakula nchini.

Aliwataka mamalishe kutumia fursa ya maonesho ya Nane Nane kupanua wigo wa biashara zao hapa nchini.

Aliwapongeza waandaaji wa maonesho hayo ambayo alisema yamefana kuliko mengine yaliyopita huku akipongeza Wizara ya Kilimo kwa usimamizi mzuri.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema kwa sasa wakulima hawapaswi kuwa na wasiwasi na kilimo wanachofanya, kwa sababu serikali iko pamoja nao kuhakikisha wanapiga hatua.

Alisema kilimo kila siku kinabadilika na kuwasihi wakulima kuwatumia maofisa ugani kupata njia sahihi za kufanya kilimo bora chenye mafanikio.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliwakaribisha wakulima na wafanyabishara hao kutumia maonesho hayo kujinufaisha ili wapige hatua.

# Washindi CRDB Marathon kuzawadiwa mil. 98.3/-

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache kabla ya wakimbiaji kushiriki msimu wa tano wa mbio za hisani za CRDB Bank Marathon 2024 zitakazoongozwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, benki hiyo imetangaza zawadi za washindi zenye thamani ya Sh. milioni 98.3 na kutambulisha jezi zitakazovaliwa na washiriki wa mbio hizo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa benki hiyo na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa amesema, mwaka huu ni msimu wa tano ambao kwa mara ya kwanza mbio hizo zinavuka mipaka ya Tanzania, na kufikia nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

"Kuvuka huku mipaka kunamaanisha kuwa Jeshi letu la Kusambaza Tabasamu (JLKT) linaendelea kukua ambapo mwaka huu malengo yetu ni kusajili jumla ya wanajeshi 8,000 hapa Tanzania, wengine 1,000 nchini Congo na 1,000 nchini Burundi. Mwitikio wa usajili ni mkubwa sana kwani nchini Congo wanajeshi wa kusambaza tabasamu 1,127 wameshajiandikishana wapo tayari kushiriki mbio hizo zitakakazofanyika Agosti 4," alisema Tully. Nchini Burundi mbio zitafanyika Agosti 11 na tayari washiriki 891 wamejisajili ili kusambaza tabasamu na anaamini idadi hiyo itaongezeka na kuvuka malengo. Tanzania watu 5,583 wamejisajili, kati ya washiriki 8,000 wanaotarajiwa kushiriki mbio hizo. Kati ya wakimbiaji waliojiandikisha, 823 wametoka nje ya nchi.

Alisema zawadi zitakazotolewa ni Sh. milioni 10 kwa mshindi wa kwanza wa kilomita 42.2 kwa wote, wanawake na wanaume huku mshindi wa pili akiondoka na Shilingi milioni tano na wa tatu Shilingi milioni mbili. Mshindi wa nne atajinyakulia Shilingi milioni moja na atakayefuata ni Sh. 500,000 wa sita ataondoka na Sh. 300,000. Benki pia itamzawadia Mtanzania mmoja wa kike na kiume atakayeshinda mbio ndefu Shilingi milioni mbili kwa kila mmoja.

Kwa watakaokimbia kilometa 21.1, amesema mshindi wa kwanza atapata Shilingi milioni tano, wa pili Shilingi milioni mbili, wakati mshindi wa tatu atapata Shilingi milioni moja.

Mshindi wa nne atajinyakulia Sh. 500,000 wa tano atapata Sh. 300,000 na wa sita Sh. 200,000. Kwa Mtanzania mmoja wa kike na kiume atakayeshinda mbio hizo, alisema atapata Shilingi milioni moja kwa kila mmoja.

Kwa washindi wengine watapata zawadi zao kama zilivyoandaliwa na benki hiyo.

Mbio hizo pia zitajumuisha waendesha baiskeli watakaoshindana umbali wa kilomita 65.

Tully alisema kutakuwa na zawadi za aina mbili, fedha taslimu pamoja na malazi katika hoteli ya nyota tano, zawadi zitakawahusu pia washindi wa mbio za kilomita 10.

Vilevile, kutakuwa na zawadi maalum kwa watoto watakaojishindia baiskeli na vifaa vya michezo ya watoto kutoka Ramohs Kids Toys yenye thamani ya shilingi milioni 1, pamoja na kufunguliwa akaunti za Junior Jumbo itakayowekwa shilingi 500,000.

Kwa wazee watakaojitokeza, washindi (mwanamke na mwanaume) watalipiwa malazi ya usiku mmoja pamoja na kifungua kinywa katika Hoteli ya Hyatt Regency kwa thamani ya shilingi milioni 1.8 pamoja na runinga chapa ya Hisense UHD inchi 43 yenye thamani ya shilingi 800,000.

Zawadi ya mwisho, itaenda kwa mshiriki wa Jeshi la Kusambaza Tabasamu atakayetokea kitofauti zaidi kimavazi ambaye atalipiwa malazi ya usiku mmoja katika Hoteli ya Hyatt Regency pamoja na kifungua kinywa. Nao pia watapata 'sound bar' chapa ya Hisense yenye thamani ya Sh. 800,000.

# Wanafunzi 360 hawajaripoti sekondari

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

ZAIDI ya wanafunzi 360 waliopaswa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2024 katika shule za sekondari Masasi mkoani Mtwara, hawajaripoti hadi sasa.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Louter Kanoni, alitoa takwimu hizo juzi wakati akizungumza kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kilichofanyika katika ukumbi wa halmashauri hiyo.

Alisema watendaji wa kata na vijiji wote wanapaswa kufuatilia kwenye maeneo yao na kuhakikisha watoto ambao hawajaripoti shuleni wanafanya hivyo na kuanza masomo mara moja.

Mkuu wa wilaya alisema inasikitisha kuona idadi kubwa ya wanafunzi hadi sasa bado hawajaripoti shuleni na wako mtaani, jambo ambalo si sawa hasa wakati huu ambao serikali imejenga miundombinu mingi ya shule na kuondoa ada.

"Watendaji wa kata naamini mnafahamu kuwa sheria iko ya mzazi au mlezi ambaye mtoto wake hajaenda shule kuanza masomo, anakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Sasa mbona nyinyi hamuitumii sheria hii?" alihoji Kanoni.

Pia alisema serikali ya wilaya ya Masasi ilishatoa maelekezo kuhusu watoto wote ambao walitakiwa kujiunga na kidato cha kwanza kuwa tayari wameripoti shuleni lakini inaonekana hali bado kwa baadhi ya wanafunzi kutii maelekezo hayo. Kanoni alisema kwa sasa kila mtendaji wa serikali anapaswa kufuatilia suala elimu kwa kufuatilia katika eneo lake kama kuna mwanafunzi ambaye hajaripoti shule kutoa taarifa ili wazazi wa mtoto huyo waweze kuchukuliwa hatua.

Alisema anashangaa kuona suala la umuhimu kwa jamii wilayani Masasi bado limekuwa changamoto kwa baadhi ya wazazi au walezi ambapo wakati mwingine mzazi hataki mtoto wake apate elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Beatrice Mwinuka, aliitaka idara ya elimu sekondari kuweka mkazo madhubuti wa kuhakikisha watoto wote ambao hawajaripoti shule wanaripoti haraka.

"Kila mtendaji kata ndani ya halmashauri yangu nataka alete orodha ya wanafunzi wote katika eneo lake ambao hawajaripoti shuleni hadi sasa mpaka wiki ijayo niwe nimeipata,"alisema Mwinuka

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ibrahimu Chiputula, alisema madiwani pia wanapaswa kukemea katika kata zao juu ya watoto kushindwa kwenda shule kuanza masomo ya sekondari hadi sasa.

Pia alisema ni muhimu kuwapa nguvu watendaji wa kata kutekeleza maelekezo ya mkuu wa wilaya ya kukamata wazazi na walezi wa wanafunzi ambao wamefaulu sekondari ila hawajaripoti shuleni.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda (kushoto), akiwa katika mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa (kulia), jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uboreshaji wa huduma kwa pamoja. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Polisi waingia shuleni kuelimisha wanafunzi

**Na Jumanne Juma**

JESHI la Polisi wilayani Bariadi limeanza kutoa elimu katika shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kutambua na kukabili matukio ya utekaji wa watoto ambayo yameshika kasi na kuzuia taharuki maeneo mbalimbali nchini.

Mkuu wa Operesheni wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Bariadi na Mkaguzi Kata ya Somanda, Mwinjuma Omary, alisema wamekuja na mkakati huo ili kuwafikia wanafunzi moja kwa moja na kuzungumza nao kutambua dalili ili wajiepushe.

Akizungumza na wanafunzi wa Shule za Msingi

Bariadi, Somanda A na B, aliwataka kuchukua tahadhari wanapoona watu wasio watambua wasikubali wawasogelee au wanapotaka kuwapa zawadi au lifti kwenye aina yoyote ya usafiri.

"Tumegundua kwa sasa baadhi ya wanafunzi wanaogopa kwenda shule, pia baadhi ya wazazi wanaogopa kuwaruhusu watoto wao kwenda shule, na wanapokwenda huku nyuma wanaishi kwa hofu kubwa. Ndio maana tumekuja kuzungumza nanyi ili mtambue na kuchukua hatua," alisema.

Alisema wimbi la watoto kupotea au kutekwa na kukutwa wamedhurika linaongezeka, ni wajibu wa kila mtoto kutokumwamini yeyote ambaye sio ndugu yake au mtu wa karibu.

Aidha, Mwinjuma aliwatoa hofu wanafunzi na wazazi kwa kuwahakikishia kuwa Jeshi la Polisi liko imara muda wote kuwalinda watoto na wananchi.

Aliwataka wanafunzi kutoa taarifa wanapoona kuna mtu au watu wanaowatilia wasiwasi ili jeshi hilo liweze kuchukua hatua mapema, huku akiwataka kutumia mbinu za kujilinda walizopewa na jeshi hilo

Wakati huohuo, Jeshi la Polisi wilayani humo limekabidhi vifaa vya usalama barabarani kwa walimu wa shule hizo, ikiwa na lengo kuwasaidi wanafunzi

kuvuka barabara katika maeneo maalumu ya kuvuka ya watembea kwa miguu.

Aidha, jeshi hilo liliwataka wale wote wanaotaka

kufanya vitendo viovu kuacha mara moja kwani wakibainika jeshi hilo litawachukulia hatua kali.

# Wakulima miwa Kilombero wapinga upotoshaji wanasiasa

**Na Mwandishi Wetu,** KILOMBERO

WAKULIMA wa miwa katika Bonde la Mto Kilombero, mkoani Morogoro, wamepinga kauli za upotoshaji zinazotolewa na wanasiasa kuwa kilimo cha miwa kimeporomoka na wakulima hawalipwi stahiki zao.

Wakizungumza na waandishi wa habari wilayani Kilombero, Mwenyekiti wa Umoja wa Wakulima wa miwa, Bakari Mkangamo aliyekuwa na viongozi wa umoja wa vyama vya wakulima pamoja na baadhi ya wakulima wanaounda vyama 17 vya ushirika (AMCOS), alisema taarifa hizo ni uzushi na upotoshaji unaofanywa kwa maslahi ya kisiasa.

"Hakujawahi kutokea bei ya miwa kushuka kwani tangu tuanze kuuza miwa msimu huu tumeuza kwa Sh. 108,000 kwa tani moja tofauti na hizi taarifa za uongo zinazosambaa," alisema.

"Mkataba wetu una kipengele cha kukaa, kujadiliana kila baada ya miezi mitatu tofauti na taarifa za uongo zinazosambaa zinazosema bei imeshuka kwa asilimia 70 kitu ambacho si kweli," alisema Mkangamo.

Wakulima hao walisema kuwa hawajawahi kutokea wakachelewesha malipo yao kwa muda mrefu na kiwanda bali huchelewa kwa siku moja au mbili kunatokana na mifumo mipya iliyowekwa iliyosogeza kutoka tarehe 15 hadi 17.

Wakulima hao walisisitiza kuwa hakuna athari zozote zilizowapata kutokana na uamuzi wa serikali kutotoa vibali vya kuagiza sukari nje kupunguza ongozeko la bei ya bidhaa hiyo ili kuleta ahueni kwa wananchi.

Meneja wa umoja huo, James Mayunga alisema wakulima wa miwa ndio wanufaika wakubwa wa sekta ya sukari na kwamba wanajua hakuna athari zozote kama inavyopotoshwa.

"Sisi wakulima tunajivunia sera nzuri za serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Sukari Tanzania zinazowafanya wakulima wa miwa wajivunie na biashara yao, tukiamini kuwa muunganiko huu utakuwa na tija kwetu," alisema.

Mmoja wa wakulima wa miwa katika Bonde la Kilombero, Tabu Lwena aliwataka viongozi wa vyama vya ushirika kutowafumbia macho wanaojaribu kupotosha kwa lengo la kuharibu sekta ya miwa. "Sisi wakulima huwa tunakaa kila mara kuangalia tunaendaje kwa maslahi ya kazi zetu, sasa hawa wanaotoka mitandaoni huko kutoa habari za uzushi wanataka kutuharibia kazi hivyo tunaomba vyama vyetu vilishughulikie jambo hili," alisema Tabu.

Iddy Luko alisema kuelekea mwaka wa uchaguzi mkuu watajitokeza watu wengi kujaribu kusambaza habari zisizokuwa na ukweli, ili wafanikiwe kupenyeza ajenda yao, hivyo ukweli kuhusu sekta ya kilimo cha miwa unapatikana kwenye vyama vya ushirika.

"Sisi tunajua wengine huko wanapitisha ajenda zao za uchaguzi ndio maana wamefika huku kwenye miwa, lakini sisi kama wakulima tunashukuru ushirikiano mzuri na mkakati wa serikali kuhakikisha sisi wakulima wa miwa tunanufaika," alisema Luko.

Wakulima hao walisema wameamua kutoka hadharani kuzungumza baada ya mbunge mmoja kueleza umma kuwa bei ya miwa imeporomoka kutokana na mabadiliko yaliyofanywa na serikali kutoa vibali vya kuagiza sekari nje ya nchi katika kukabili uhaba.

Kwa mujibu wa wakulima hao, vyama vyao vya ushirika vina ushirikiano mkubwa na Kiwanda cha Sukari cha Kilombero katika biashara hiyo kiasi cha kupata matumaini makubwa ya mageuzi ya zao hilo, hasa kutokana na mikakati ya kiwanda kulenga kufanya upanuzi mkubwa utakaowafanya wakulima wauze miwa yao kwa wingi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hitilafu ya umeme treni ya SGR iiamshe TRC kuimarisha miundombinu

**JUMANNE** wiki hii, usafiri wa treni ya reli ya kiwango cha kimataifa (SGR), maarufu kama treni ya mwendokasi, ulisimama kwa saa mbili katika stesheni ya Kidete na Kilosa ikiwa njiani kwenda Dodoma, sababu iliyotolewa ni hitilafu ya umeme iliyotokana na ngedere na bundi baada ya kuchezea nyaya za umeme zilizotandazwa juu ya reli.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kitengo cha Uhusiano cha Shirika la Reli Tanzania (TRC), hitilafu hiyo ilisababisha umeme kukatika katika kituo cha kupooza umeme namba saba kilichoko Godegode majira ya saa 4:20 usiku.

Baada ya hitilafu hiyo, taarifa hiyo ilisema mafundi wa TRC walitatua changamoto hiyo na kurejesha umeme saa 6:30 usiku. Hivyo, kuwezesha treni hiyo kuendelea na safari ya kwenda Dodoma na kuwasili saa 7:57 usiku. Kutokana na tatizo hilo, TRC imeomba radhi kwa wateja kwa sababu ya usumbufu uliojitokeza.

Kuwapo kwa tatizo hilo, kuliibua mjadala kwenye mitandao ya kijamii huku wadau wakirejelea kauli iliyowahi kutolewa Mei, 2020 na Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, kwamba treni hizo zitakuwa na uwezo wa kutumia mafuta, lakini zina uwezo wa kuhifadhi umeme endapo utakatika.

Zaidi ya kuhoji hivyo, baadhi walichukua picha za bundi na ngedere na kuwavika vikoti vya kuakisi mwanga wakionekana wako kwenye mitambo ya reli wakiwa wameshikilia vifaa vya kukatia umeme wakati treni ikiendelea na safari. Utani mwingine mtandaoni ni ulioonesha picha ya treni na juu yake kukiwa na ngedere na bundi zikiwa na maelezo yanasomeka: "Ngedere na bundi watatiza usafiri wa SGR nchini Tanzania."

Kwa ujumla, tatizo hilo limeibua maswali mengi ambayo baadhi yake hayana majibu ya moja kwa moja kuhusu usalama wa usafiri huo ambao ujio wake ulielezwa kuwa mkombozi kwa Watanzania wengi hususani maeneo ambayo treni hiyo itakuwa inapita baada ya kukamilika. Watu waliouona usafiri huo kuwa, ni muhimu kwa sababu unatumia muda mfupi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ukilinganisha na ule wa mabasi.


Kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro, mathalan kwa usafiri wa treni ni saa moja na nusu (dakika 90) wakati hadi Dodoma ni saa tatu na nusu. Kwa basi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ni saa nne na hadi Dodoma ni saa nane hadi 10.

Kwa ulinganifu huo wa muda kati ya usafiri wa basi na treni ya SGR, muda mwingi unaokolewa mtu anapotumia treni ya mwendo kasi na anaweza kufanya mambo yake tofauti na muda ambao anatumia kwa basi. Mtu mmoja aliwahi kusema anaweza kukaa Morogoro na kufanya shughuli zake Dar es Salaam au vinginevyo kwa sababu ya neema hiyo ya usafiri wa treni ya SGR.

Pamoja na hitilafu hiyo, usafiri huo uliozinduliwa jana na Rais Samia Suluhu Hassan, bado ni mkombozi kwa watu wengi kwa kuwa unachukua muda mfupi na hata kuokoa gharama mbalimbali.

Wahenga wanasema kuwa, gunia la sukari haliwezi kubadilisha ladha ya maji katika bahari, hivyo kinachotakiwa ni kwa TRC kuelimisha umma kwamba hilo ni tatizo la kiufundi linaloweza kutatuliwa na usafiri huo kuendelea kuaminiwa na Watanzania wengi na hata kuwa sehemu ya utalii wa ndani.

Aidha, tukio hilo limetokea alfajiri ukilinganisha na muda wa treni hiyo ilipoanza kutoa huduma, hivyo makosa yameonekana mapema na yanaweza kurekebishwa haraka. Kwa mantiki hiyo, umakini zaidi na ulinzi katika miundombinu hiyo unapaswa kutiliwa manani kwani huenda ngedere na bundi wametoa tahadhari ya mapema kwamba lolote linaweza kutokea na TRC hawapaswi kujiamini kwamba mambo yataendelea kuwa shwari siku zote.




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuzindua SGR Rais pokea maua yako

Na Moshi Lusonzo

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, amezindua rasmi reli ya umeme , wengine wakiita ya mwendokasi au ya kisasa ama SGR . Yote ni majina yake. Mama anaifanya Tanzania kuingia katika zama mpya za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia treni za kasi. Pokea maua yako.

Ni mataifa machache ya Afrika Kusini ya Jangwa Sahara yenye treni za umeme. Hivyo Tanzania Nigeria, Ethiopia, Djibouti na Kenya ni mataifa machache yenye reli hiyo.

Kimsingi hatua hiyo ni ya kupongezwa hasa kutokana na juhudi za Rais Samia na serikali yake kutenga fedha nyingi katika kukamilisha ujenzi wa reli, ununuzi wa mabehewa na vichwa vya treni.

Wizara ya Ujenzi inasema treni hiyo imeanza kutoa huduma mwezi uliopita kuanzia Dar es Salaam- Morogoro na hatimaye Dodoma, jumla ya abiria 8,000 wanasafiri kwa kutumia usafiri huo kila siku.

Pamoja na mazuri yanayoonekana baada ya kuanza kwa usafiri wa treni ya mwendo kasi, kuna baadhi ya dosari zinajitokeza ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi.

Moja ya dosari ambayo hata rais mstaafu Jakaya Kikwete, anaizungumizia ni uchache wa vituo vya treni hiyo na kusababisha baadhi ya maeneo muhimu kushindwa kufikika ipasavyo. Kuna maeneo mengi ya miji au yale ya uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na madini anasema hayana vituo vya treni na kusababisha usafiri huo kutoonekana umuhimu wake katika maeneo hayo.

Dosari nyingine ni ile ya juzi ya treni kusimama kwa zaidi ya saa mbili baada ya umeme kukatika lawama zikielekezwa kwa wanyama wanaodaiwa kugusa nyaya za umeme.

Kukosekana kwa udhibiti wa wanyama na ndege katika njia za umeme zinazopita kati ya mapori na hifadhi kunaweza kusababisha imani ya wasafiri wa SGR kupungua.

Tukio hilo ni funzo kwa kampuni ya reli na pia kutoa ujumbe kwamba wanatakiwa kuangalia namna bora zaidi ya kudhibiti matukio kama hayo ili huduma hiyo ionekane ya uhakika, ya weledi na yenye usalama.

Wizara na kampuni inayosimamia usafiri huo wana wajibu wa kutoa elimu na usaidizi kwa wananchi wanaoishi jiriani na njia ya reli kuangalia na kuitunza miundombinu hiyo ikiwamo kutoa taarifa za uharibifu kama huo ili kupunguza hasara.

Dosari nyingine ambayo watu waliotumia usafiri huo wameonekana kutilia shaka, ni namna abiria asivyoruhusiwa kuingia na mzigo usiozidi kilo tano.

Ni jambo zuri kudhibiti mizigo mingi na uchafu ili kudumisha usafi na kuweka viwango, lakini uongozi wa kampuni ya reli na wizara vingetafuta njia mbadala ya kubeba mizigo kiasi pengine hata kilo 50 ili kuwapa nafuu watu kusafiri na kiasi cha mizigo badala ya mkoba na koti mkononi bila zawadi kwa wana familia au watoto wao wanaowapokea vituoni.

Ikumbukwe kuwa mikoa ambayo treni hiyo imeanza safari zake inafahamika kwa uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula, mboga na matunda, hivyo kutokana na treni hiyo kutumia muda mchache kufika kituo kimoja hadi kingine kuna umuhimu wa kujengwa nyumba au ghala za kuhifadhia mazao ya kilimo.

Wakati safari zikiongezwa kwa treni nyingine ya mizigo hivi karibuni, vituo vya kuhifadhi mazao ya kilimo hasa mboga, mazao mabichi, mboga, ndizi, mihogo na matunda na kwa kila kituo ni suala muhimu na halipaswi kupuuzwa.

Kwa mfano wakulima wa mboga wa Morogoro na zabibu kutoka Dodoma, wawe na uhakika wa kusafirisha na kuuza mazao yao bila kuharibika.

Kila kituo chenye uzalishaji huo kwa wingi kijengwe vyumba au maghala ya baridi (cold rooms) kutunzia vyakula vinavyoharibika haraka, kwani mkulima anapofikisha shehena yake asiwe na hofu kupoteza nguvu yake hata kama usafiri kwa siku huo utaahirishwa kutokana na sababu mbalimbali.

Pamoja na yote, ni lazima serikali ione namna bora ya kushirikisha wawekezaji kuboresha uzalishaji wa bidhaa mbalimbali pembeni ya reli kukuza uchumi wa mikoa na sehemu inapopita SGR.

Wakati wananchi wanaungana kwa pamoja kuipongeza serikali ya awamu ya sita kwa kufikia ndoto hiyo ambayo viongozi waliotangulia walianzisha utekelezaji wake na hatimaye mwaka huu imefikiwa, wakumbuke mlinda nchi ni mwananchi. Watunze reli lisiwe eneo la kukata na kuiba nyanya za uzio na matendo mengine ya hujuma.

Tumpe Rais Samia maua yake kutokana na juhudi zake na kuvuka vikwazo mbalimbali mpaka kuhakikisha mradi huu mkubwa unakamilika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

# Watoto wa Kusini mwa Sahara hatarini kutofikia hatua za ukuaji

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

THELUTHI mbili ya watoto chini ya miaka mitano walio kusini mwa Jangwa la Sahara, wako hatarini kutofikia hatua zao za ukuaji.

Inaelezwa kuwa katika watoto milioni 250 wenye umri wa miaka chini ya mitano duniani wako hatarini kutofikia hatua zao za ukuaji. Kati yao, asilimia 66 wako Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Edna Katalaiya alibainisha hayo juzi wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa mkoa huo.

Katalaiya alisema zipo changamoto katika uwekezaji katika malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto wa miaka 0-8, shida kuu ikiwa ni kutopewa uzito unaostahili; badala yake msisitizo umewekwa katika kupunguza vifo.

Alisema kipindi cha miaka 0-8 ni fursa muhimu ya kuboresha maendeleo ya binadamu na hivyo kupata mtaji bora wa rasilimali watu wenye tija.

Kaimu Katibu Tawala huyo pia alitoa maelekezo kwa halmashauri za mkoa huo kuendeleza kutekeleza programu hiyo sambamba na kutenga bajeti na kufanya tathmini kila robo mwaka kwa kujipima utekelezaji.

Christopher Peter ambaye ni mwezeahaji wa masuala ya watoto kutoka Shirika la Tecden, alisema udumavu kwa watoto nchini kwa sasa ni asilimia 30 huku Mkoa wa Pwani ukiwa na asilimia 20.

Akizungumzia masuala ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, Peter alisema wanaume wanatakiwa kuweka utaratibu wa kuambatana na wenzake wao kwenda kliniki ili washiriki moja kwa moja katika malezi na makuzi ya watoto wao badala ya kuacha kazi hiyo kufanywa na mwanamke pekee.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Kusirye Ukio alipongeza juhudi zinazofanywa na wizara na wadau wa maendeleo katika utekelezaji programu hiyo ambayo anaamini italeta mabadiliko katika malezi ya watoto.

Programu hiyo kwa Mkoa wa Pwani inatekelezeka kwa kushirikiana na serikali, taasisi ya Anjita, shirika la Tecden, Children in Crossfire sambamba na Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Manzi Rwegasira (kushoto), akikabidhi cheti kwa Ruthbrenda Kundasen aliyehitimu mafunzo maalumu ya benki hiyo yenye lengo la kuwaandaa wafanyakazi vijana kuwa viongozi wajao katika taasisi za kifedha, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali watu wa benki hiyo, Rabina Masanja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT: Umiliki wa ardhi umulikwe kuimarisha usalama wa wananchi

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI wakuu wa ACT Wazalendo wamesisitiza msimamo wa chama hicho kutaka Wizara ya Ardhi ivunjwe na kuondoa mfumo wa umiliki wa ardhi katika mikono ya Rais, wakiamini kutadhibiti

serikali kuhodhi ardhi nchini.

Vilevile, viongozi hao wamesisitiza dhamira ya kupigania umiliki wa ardhi uwekwe kikatiba ili kuimarisha usalama wa ardhi ya wananchi.

Hatua hizo za kukabiliana na wimbi la migogoro na uporaji wa ardhi zilielezwa na viongozi wa chama hicho juzi katika mwendelezo wa ziara ya chama mikoa 22 na majimbo 125 wakiwa Buhigwe (Kigoma), Ngorongoro (Arusha), Ukerewe (Mwanza) na Newala

Vijijini (Mtwara).

Makamu Mwenyekiti Bara, Isihaka Mchinjita alikosoa vikali utaratibu mpya ulioanzishwa wa kodi ya ardhi kwa makundi yote ya ardhi (ardhi ya kijiji na ardhi ya jumla).

Alisema ACT Wazalendo inapinga vikali utaratibu huo wa kodi ya ardhi kwa kuwa utapalilia uporaji ardhi ya wananchi kutokana na utekelezaji sheria hiyo.

"Inashangaza wazee wetu walipigania uhuru, sijui wa nini? Kodi ya Ardhi ya Kijiji ni kwa ajili ya maslahi ya nani? Hii ni mbinu tu wanataka ukishindwa kulipa kodi wakupore na kukunyang'anya ardhi yako. Tutasimama kupinga utekelezaji sheria dhalimu ya namna hii," alisema Mchinjita.

Mchinjita pia alitaka Wizara ya Ardhi ivunjwe na kuundwa upya ili kutenganisha usimamizi wa sera na masuala ya kiufundi na utekelezaji.

Badala yake, Mchinjita alisema wanataka kiundwe chombo kitakachosimamia masuala ya ufundi na utekelezaji ili kuondoa siasa kwenye upimaji, umiliki na mipango ya ardhi nchini na kutaka gharama za upimaji

zibebwe na serikali.

Katibu Mkuu wa Chama, Ado Shaibu, akiwa Nansio jimboni Ukerewe, alisema vyombo vya utatuzi wa migogoro vimeshindwa kutekeleza majukumu yake.

Hivyo, alitoa wito wa kuboreshwa vyombo hivyo ili kumaliza migogoro ya ardhi nchini.

"Migogoro ya ardhi inazidi kuongezeka na mingine haijatatuliwa kwa miaka mingi, yote hii ni kwa sababu mifumo yetu ya utatuzi wa migogoro kutofanya kazi vizuri.

"Serikali iliagiza mawaziri kuzunguka, haikusaidia! Serikali inapaswa kuanzisha mahakama zinazotembea katika ngazi ya wilaya (circuit courts) ili zitatue

migogoro ya ardhi katika maeneo husika badala ya maigizo ya kuwapeleka mawaziri, tena kwa gharama kubwa," alidai.

Katibu Mkuu pia alisema kuwa ili kushughulikia migogoro, ni muhimu mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji yaimarishwe, kusimamiwa na kujengewa uwezo ili yaweze kushughulikia, kuamua na kutatua masuala ya ardhi katika maeneo yao kwa wakati.

Kiongozi wa Chama mstaafu, Zitto Kabwe akizungumza na wananchi wa Jimbo la Buhigwe (Kigoma), alisema ACT Wazalendo ikishika madaraka itarejesha na kugawa upya ardhi kwa wananchi walioporwa na kunyang'anywa na serikali.

"Ardhi ni uhai, ardhi ni maendeleo! Serikali inapochukua ardhi yenu maana yake inataka kuwafanya wananchi muwe masikini kwa kuwageuza kuwa manamba kwenye ardhi yenu wenyewe.

"Wameweka ushuru, tozo, kodi... sasa wanaona

haitoshi wanataka kuchukua ardhi yote! ACT Wazalendo tumedhamiria kuilinda ardhi yenu na ahadi yetu kwenu tutarejesha ardhi yote iliyoporwa," alisema Zitto.

Kiongozi wa Chama, Dorothy Semu, akiwa jimboni Ngorongoro (Arusha) alisema ardhi kuwekwa kwenye mikono ya Rais ndio kiini cha matatizo yaliyopo, yakijumuisha vipigo kwa wananchi wa Loliondo, Ngorongoro na maeneo mengine nchini.

"ACT Wazalendo tunataka milki ya hatma ya ardhi iondolewe mikononi mwa Rais na kupelekwa kwenye chombo chenye uwakilishi wa wananchi (Bunge na Mkutano Mkuu wa Kijiji)," alisema Dorothy.

Aliongeza kuwa sheria za ardhi zinachezewa na serikali na hivyo kurahisisha uporaji. Ili kuongeza ulinzi wa ardhi na kudhibiti viongozi wasiojali maslahi ya nchi, Dorothy alisisitiza kwamba ardhi inapaswa kuwekwa kikatiba na ACT Wazalendo itapigania hilo.

Akizungumzia utaratibu wa fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya maendeleo, alisema ACT Wazalendo inaitaka serikali kuanzisha utaratibu endelevu wa wananchi kunufaika na ardhi ya uwekezaji iliyotwaliwa kwa kupewa sehemu ya umiliki wa mradi (Land for Equity).

Ziara ya chama inayokusudia kufikia mikoa na majimbo yote ya Tanzania Bara inaendelea katika

majimbo ya Nkasi (Rukwa), Ukerewe (Mwanza), Tandahimba (Mtwara) na Loliondo (Arusha). Ni ziara inayolenga kusimamia uwajibikaji wa serikali kuhusu kero za wananchi, kusajili wanachama kwenye mfumo wa kielektroniki na kukiandaa chama na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Wastaafu Posta wavutana malipo SACCOS

Na Enock Charles

IKIWA ni miaka zaidi ya 10 ya wastaafu zaidi ya 1,000 wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania kudai stahiki zao katika Chama cha Kuweka na Kukopa cha Posta na Simu SACCOS, mvutano umeibuka kuhusu kiasi cha madai baina yao na uongozi wa sasa wa chama hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Meneja wa Posta na Simu SACOSS, Essau Mwasilembo, alisema wastaafu hao wanadai Sh.bilioni moja na si Sh. bilioni tisa kama wanavyoeleza kwenye vyombo vya habari.

Aidha, alithibitisha kuwa madai hayo ni ya muda mrefu na kuomba chama kupewa muda ili kuyalipa.

"Nitumie fursa hii kuwaomba wastaafu waendelee kutuvumilia uongozi upo pamoja nao na unafanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba unatatua tatizo hili," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wastaafu hao, David Hango, aliwaambia waandishi wa habari kuwa licha ya kuwasilisha madai yao kwa viongozi mbalimbali wa serikali, mpaka sasa hawajafanikiwa kulipwa fedha zao huku wengine wameshafariki dunia bila kupata stahiki zao.

Akifafanua madai yao alisema, ipo michango ya kila mwezi waliyokuwa wakichanga kipindi chao cha utumishi katika lililokuwa Shirika la Posta na Simu ambapo baadaye vilitenganishwa na kupatikana Shirika la Posta na Shirika la Simu na hivyo kuwapo akiba ya wanachama inayofikia Sh. bilioni 1.2.

Pia alisema zipo hisa katika Benki ya TCB ambazo alidai zinafikia Sh. bilioni tatu na hisa za majengo ya Posta ya Sh. bilioni tano.

"Mwaka 2019 tulikwenda kwa Meneja wa Chama cha Kuweka na Kukopa (KK) na kumtaka alipe stahiki zetu, lakini cha ajabu alisema chama hakina fedha za kulipa mpaka kiuzwe kiwanja ambacho ni mali ya chama kilichopo Mabibo," alisema Hango.

Mwenyekiti huyo alisema kuendelea kusubiri mpaka mali fulani iuzwe katika chama ndipo walipwe ni kinyume cha katiba yao aliyodai inataka mtu akistaafu kulipwa ndani ya muda wa siku 90 na kwamba wamesubiri kwa miaka zaidi ya 10 huku wengine wakiwa wameshafariki dunia bila kulipwa stahiki zao.

"Utaratibu wa kusema tusubiri mpaka kitu fulani kiuzwe ndipo tulipwe ni kinyume cha katiba yetu na pia hakuna ushirikishwaji katika hilo mambo yanafanywa kimyakimya," alidai Hango.

# Uhakika mawasiliano vijijini kuchochea kasi maendeleo

Na Maulid Mmbaga

WADAU wa maendeleo nchini wamesema kuwa jitihada zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi katika ufikishaji wa mawasiliano vijijini umesaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa haraka wa huduma za kijamii hususani uimarishaji elimu wezeshi kidijiti na afya.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), inaeleza kuwa hatua hiyo inachangia kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Taifa ya 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa miaka mitano (FYDPIII) na Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali utakaotekelezwa kati ya 2024 na 2034.

Kwa mujibu wa TCRA, dira ina mikakati ya kuendeleza mawasiliano kwenye ngazi zote, kujenga uchumi wa kidijiti na kuwa uchumi huo utawezeshwa kwa kuimarisha mwelekeo tawala wa matumizi ya TEHAMA kwenye sekta zote.

"Ukuaji wa teknolojia ya mawasiliano nchini hasa maeneo ya vijijini umesaidia pia ufikishaji wa taarifa kwa wakati, uendeshaji wa masuala mbalimbali ya kijamii, kuchochea maendeleo na biashara, uzalishaji na ukuaji wa uchumi kwa ujumla," ilisema.

Ripoti ya TCRA ya hali ya mawasiliano ya robo mwaka iliyoishia Juni, ilionesha kuwa miongoni mwa kampuni za mawasiliano ambazo zimefanikisha upatikanaji wa huduma ya mtandao vijijini ni Airtel, takwimu zakionyesha kuwa imevifikia zaidi ya vijiji milioni 5.8 sawa na asilimia 53.

Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Africa, Sunil Taldar, alisema ufikishaji wa mawasiliano vijijini umewapa mafanikio mbalimbali ikiwamo kuongeza wateja wa mawasiliano ya simu ya mkononi milioni 155.4 sawa na asilimia 8.6.

Alisema mafanikio hayo yanaonesha ukuaji endelevu katika msingi wa wateja wao na matumizi, akieleza kuwa utendaji bora unawawezesha kupata fursa mbalimbali zitakazowawezesha kupiga hatua kwenye tasnia ya mawasiliano.

"Kipaumbele muhimu kwetu ni kutafuta fursa mpya za kukua. Tutajenga msingi imara iliyoanzishwa kwa miaka mingi ili kutoa fursa hizi mpya za kibishara kwa watanzania. Muhimu zaidi, msisitizo wetu ni kuboresha kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika jamii," alisema Sunil.

Ripoti ya TCRA ilisema kuwa sekta ya mawasiliano imepata maendeleo na ongezeko kubwa la kupitishwa kwa huduma za mawasiliano ya simu, kutokana na kuendelea kwa ushindani wa ushuru wa huduma, na kwamba mafanikio makubwa yalikuwa upanuzi mkubwa wa mtandao wa simu za mkononi.




Mkuu wa Polisi wilaya ya Kipolisi Mabwepande (OCD) Colle Mshauri, akiwa ameshika tuzo baada ya kutunukiwa na Umoja wa Madereva Bajaji Bunju (UMABABU), kutokana na utendaji kazi wake mzuri katika kuhudumia wananchi, wakati wa hafla ya kuadhimisha miaka miwili ya umoja huo, Bunju, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali kushughulikia mgogoro wa ardhi Rusumo

Na Judith Julius, NGARA

SERIKALI imepokea malalamiko ya mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na Jeshi la Magereza katika Kijiji cha Rusumo, wilayani Ngara mkoani Kagera.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, alisema hayo wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Rusumo, wilayani Ngara mwishoni mwa wiki baada ya kufanya ziara ya kikazi ya kufuatilia mgogoro baina ya wananchi na Jeshi la Magereza.

Sillo alisema serikali ni sikivu na suala hilo atalifikisha katika vikao vya kamati ya maamuzi ili liweze kutatuliwa.

"Niwaombe wakazi wa kata na kijiji hiki cha Rusumo kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anawapenda sana na sisi kama wizara tumewekwa kwa ajili kumwakilisha yeye ili kutatua changamoto zenu, suala hili la mgogoro huu nimelichukua na tutalishughulikia," Sillo alisema.

Awali, Mbunge wa Jimbo la Ngara, Ndaisaba Ruhoro, alisema mgogoro huo umedumu kwa zaidi ya miaka 18 na umekuwa kikwazo katika utekelezaji wa shughuli za uzalishaji mali.

"Mgogoro huu umedumu kwa zaidi ya miaka 18 sasa nikuombe utusaidie kwani wananchi wanakumbana na changamoto mbalimbali nakushindwa kufanya shughuli zao za uzalishaji mali ili kujiinua kiuchumi," Ruhoro alisema.

Katika hatua nyingine, Sillo alisema Serikali ya Tanzania imetenga dola milioni 100 kwa ajili ya kununua magari ya Zimamoto na uokoaji hapa nchini ili kukabiliana na majanga ya moto.

"Eneo hili la kituo cha forodha cha mpaka wa Rusumo ni eneo muhimu kwa ajili ya uchumi wa taifa letu na linahudumia nchi jirani ya Rwanda, hivyo ni muhimu kuwa na vifaa vya utayari kwa ajili ya uokoaji pindi majanga yanapotokea," Sillo alisema.

Alitoa kauli hiyo baada ya kutembelea kituo cha forodha cha mpaka wa Rusumo na kuambiwa na Mbunge wa Jimbo la Ngara, Ruhoro, kuwa katika eneo hilo kumekuwa kukitokea ajali za malori kuwaka moto, lakini hakuna gari la Zimamoto pamoja na vifaa vya uokoaji.

"Hapa katika eneo hili la Rusumo kuna miteremko mikali na miinuko kama ulivyojionea mwenyewe na kila baada ya siku tatu kumekuwa kukitokea ajali za magari kuanguka wakati mwingine kuwaka moto, hivyo kutokuwapo gari la Zimamoto na vifaa vya uokoaji tunalazimika kuomba kwa jirani zetu," Ruhoro alibainisha.



# Mkenda: Utafiti utasaidia kuongeza kilimo chenye tija

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, amesema tija ndogo katika kilimo cha mazao, haiwezi kumalizwa na sekta ya ushirika pekee bali ni lazima ufanyike utafiti wa namna bora ya kufanya kilimo chenye tija.

Akizungumza jana katika mkutano wa kimataifa wa maendeleo endelevu ya ushirika mjini hapa, Prof. Mkenda, alisema katika maeneo mengi, ushirika unaweza kusaidia wakulima wadogo kulima kwenye shamba moja kubwa na kuuza kwa tija.

Mkutano huo wa siku tatu unaendelea katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), ukiwashirikisha wanazuoni pamoja na wadau mbalimbali kutoka nchi za Tanzania, Kenya, Botswana, Ethiopia, Nigeria, Eswatini, Finland na India.

"Tunatambua mchango mkubwa wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi katika sekta ya ushirika nchini; lakini pia tunakishukuru kwa kuandaa mkutano wa kimataifa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika cha Kenya.

"Tungependa kusisistiza vyuo vikuu kwamba, haviwezi kuwa ni vyuo vikuu kama vinajifungia ndani tu. Lazima viwe na ajira ya wakufunzi kutoka nje ili na Watanzania wengine wakafundishe nje, washirikiakene katika masuala ya utafiti."

Kwa mujibu wa Waziri Mkenda, licha ya mkutano huo kujadili mambo ya ushirika, serikali imesisitiza mageuzi ya elimu nchini, yanavisukuma vyuo vikuu vingine vifanye shughuli ambazo ni za amali, kwa kuwa ushirika ni aina fulani ya mafunzo ya amali.

"Nimejaribu kuwahimiza wanataaluma hawa, kuangalia namna ya kutumia ushirika kutatua changamoto katika kilimo na uchumi wa vijijini.

"...Takribani theluthi mbili ya watu wetu wanafanya shughuli za kiuchumi vijijini, kwa Tanzania asilimia 58 ya nguvu kazi inafanya shughuli vijijini; na hasa shughuli za kilimo na mazao, lakini hao theluthi mbili wanachangia chini ya theluthi moja ya pato la taifa."

Kilimo cha mazao kinachangia kwa Tanzania, asilimia 15 ya pato la taifa.




Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo akizungumza wakati wa ibada maalumu ya shukrani na uzinduzi wa ujenzi wa taasisi ya matibabu ya kibingwa ya Moyo katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, mjini Moshi mapema wiki hii, iliyoongozwa Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Askofu Dk. Alex Malasusa (wa tano kulia). Ujenzi wa taasisi hiyo, utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 25 hadi kukamilika kwake. **PICHA: JAMES LANKA**

# TAKUKURU yaanzisha uchunguzi miradi minne

**Na Oscar Assenga,** LUSHOTO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Tanga, imeanzisha uchunguzi wa miradi minne iliyobainika kuwa na mapungufu ilipozinduliwa wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru 2024.

Ofisa Uchunguzi Mwandamizi wa taasisi hiyo Mkoa wa Tanga, Frank Mapunda, akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi wao kwa kipindi cha kuanzia Aprili hadi Juni 2024 kwa niaba ya Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tanga, alisema kwamba waliendelea na ufuatiliaji utekelezaji wa miradi ya maendeleo 79 yenye thamani ya Sh. 34,517,081,773.60.

Mapunda ambaye pia ni Mkuu wa Dawati la Elimu TAKUKURU Mkoa wa Tanga, alisema miradi ambayo ilifuatiliwa ni katika sekta za kipaumbele ambazo ni elimu, barabara, maji na afya pamoja na iliyotembelewa na kuzinduliwa au kuwekwa mawe ya msingi katika mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2024.

Aliitaja miradi hiyo ni ujenzi wa nyumba ya walimu katika Shule ya Msingi Kisinga, Halmashauri ya Lushoto wenye thamani ya Sh.milioni 50, Ujenzi wa Zahanati ya Milingano wenye thamani ya Sh. milioni 553,

Mapunda alitaja mradi mwengine ni upanuzi wa Kituo cha Aya Mgwashi chenye thamani ya Sh. milioni 500 na mradi wa zahanati ya Maalie wenye thamani ya Sh. milioni 50.

Wakati huo huo, Mapunda alisema kwamba katika kipindi hicho walifanya kazi ya uelimishaji kwa wajumbe wa kamati za Afya ya Msingi katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali pamoja na watumishi na wataalamu wa sekta ya afya ambao ni 485 kwa idadi yao katika wilaya za Kilindi, Handeni, Korogwe na Lushoto.

"Katika uelimishaji huo tuliweka kipaumbele ushirikishwaji wadau katika uzuiaji rushwa kwa kushirikiana na wakurugenzi wa halmashauri zote katika wilaya hizo ambapo wakuu wa wilaya zote walishiriki kufungua mafunzo na kuhimiza uadilifu, uwajibikaji na huduma bora za afya ya msingi katika wilaya zao,"alisema.

Hata hivyo, alisema kwamba wataendelea kufanya udhibiti na uzuiaji wa rushwa kwenye eneo la ukusanyaji mapato kwa kushirikiana na mamlaka husika kufanya ufuatiliaji wa moja kwa moja kwenye vyanzo vya mapato vilivyoanishwa katika bajeti kwa kuangalia mienendo ya makusanyo ya mapato sambamba na kushauri hatua mbalimbali za kudhibiti upotevu wa mapato wakati wa mchakato wa ukusanyaji.

# Kukamilika jengo la huduma ya mama, mtoto kwaleta neema

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya wanawake 15,000 wakazi wa Njiro na maeneo ya jirani jijini Arusha mkoani hapa,watanufaika na upatikanaji wa huduma bora za matibabu baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Kituo cha Afya cha Themi.

Katika ujenzi huo, serikali imetoa Sh.milioni 200 kwa ajili ya kujenga jengo hilo, ambalo limejengwa kwa mfumo wa ghorofa na liko katika hatua za awali za ujenzi.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Charles Sululu, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ujenzi huo, ikiwa ni ziara ya viongozi wa serikali na Chama Cha Mapinduzi Kata ya Themi.

Alisema mradi huo ukikamilika utawawezesha kina mama kujifungua salama, pamoja na kupata huduma hiyo, karibu na makazi yao, badala ya kwenda kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

"Mradi huu ni mkubwa utaweza kuwasaidia kina mama kujifungua salama na wakazi wengi wanaozunguka eneo hili, hivyo kurahisisha huduma kwa wanawake kutokwenda umbali mrefu kufuata matibabu kwa kuwa tutakuwa na uwezo wa kufanya upasuaji na huduma nyingine za Watoto." Alisema Dk. Sululu. Diwani wa Kata ya Themi, Lobora Ndarpoi, alisema awali kina mama walipotaka kujifungua iliwalazimu kwemda kwenye Hospitali ya Mount Meru.

"Jengo hili tumepewa Sh. milioni 200 na serikali na litakuwa msaada mkubwa kwa wananchi wetu kwa kuwa sehemu inayotumika kwa sasa haitoshelezi mahitaji,"alisema Diwani Ndarpoi.

Mwenyekiti wa Juimuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Kata ya Themi, Agness Mushi, aliipongeza serikali kwa kutoa fedha hizo ambazo zimesaidia kuongeza wigo wa utoaji wa huduma kwenye kituo hicho.

Katibu wa CCM Kata ya Themi, Deus Kitinde, alisema ujenzi huo ni utekelezaji wa ilani ya CCM, kama chama kilivyoahidi kwa wananchi mwaka 2020.

"Tunaishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za ujenzi wa mradi huu, ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya chama kama kilivyoahidi kwa wananchi mwaka 2020,"aliongeza Katibu huyo.





# Wanafunzi wasoma katika darasa lisilo na paa

**Na Vitus Audax,** RORYA

WANAFUNZI wa darasa la awali na la kwanza katika Shule ya Msingi Bubombi, Kata ya Buhura, wilayani Rorya, mkoani Mara wanalazimika kusoma katika darasa moja lisilo na paa kutokana na shule hiyo kukabiliwa na uhaba wa madarasa.

Inaelezwa kuwa shule hiyo yenye wanafunzi 1,002, awali wanafunzi wa madarasa hayo tajwa walikuwa wakisoma nje ya darasa, walimu wakitumia vibao vya kuhamishika, lakini hivi sasa wanasoma katika darasa hilo lenye ubao lakini halina paa.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Gorge Opio, darasa hiyo lilijengwa mwaka jana kwa nguvu za wananchi. Licha ya kuomba fedha serikalini kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wake, halijatengewa fedha hizo na kufanya wanafunzi hao kuendelea kulitumia hivyo hivyo.

"Serikali inasema mipango yake haijawa vizuri, lakini tunaamini pia na wao wanaona tatizo hili, kulingana na hali halisi ya jengo hatuna namna wanafunzi wa chekechea na la kwanza wanalazimika kusomea humo kwani tuna upungufu mkubwa wa madarasa.

"Tuliona tusiendelee kuwaweka nje wanafunzi na vibao vya kuhamishahamisha, hivyo tukasema waendelee kusomea humu huku tukiendelea kuwaomba wadau mbalimbali pamoja na vikundi kutusaidia kwa lolote ili tulikamishe jengo hili," alisema Mwalimu Mkuu Opio.

Alisema shule hiyo ina wanafunzi 1,002 ambako kati yao, wanafunzi wavulana ni 400 na wasichana ni 602, ikiwa na vyumba saba vya madarasa.

Mwalimu Opio alifafanua kuwa kati ya vyumba hivyo, sita vinatumiwa na wanafunzi na chumba kimoja cha darasa kinatumiwa na walimu kama ofisi.

Alisema kuwa ofisi ya walimu iliyokuwapo, ilibomoka wakati wa mvua kubwa; wana uhitaji wa madarasa 16 kuwa na ufanisi katika ujifunzaji na ufundishaji.

Mkazi wa Kijiji cha Bubombi, Meshack Zacharia alisema wamekuwa wakishuhudia wanafunzi hao wakisoma katika jengo hilo lisilo na paa hata wakati wa jua kali na kuwa boma hilo walijenga vijana wazaliwa wa eneo hilo, akiomba wadau wengine kujitokeza kusaidia ukamilishwaji wa ujenzi wake.

Alimwomba diwani wao kuweka shinikizo serikalini ili kuhakikisha wanapaua jengo hilo na kuwanusuru wanafunzi kusoma katika mazingira rafiki.

Ofisa Elimu wa Kata ya Buhura, Samson Masekemase alisema tatizo hilo ndani ya kata yake haliko katika shule hiyo pekee, bali shule zote zina uhaba wa madarasa, pia zina maboma yanayohitaji fedha za kumalizia ujenzi wake.

Alisema kata hiyo ina shule za msingi nane na mbili za sekondari, zote zinayo maboma ambayo hayayohitaji fedha kumalizia ujenzi.

"Tumeendelea kutoa taarifa serikalini juu ya maboma yaliyopo na tathmini ya fedha inayohitajika, hivyo tunategemea kutengewa fedha na serikali ili tukamilishe maboma yetu, tunajua changamoto zipo nyingi, si kwa hapa tu na shule nyingine," alisema Masekemase.

Mtaalamu wa Malezi na Makuzi ya Awali, Joel Elphas, Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la TECEC, akizungumza na Nipashe kuhusu athari za kielimu, kisaikolojia na kiafya wanazoweza kukabiliana nazo watoto wa awali na darasa la kwanza kwa kusoma katika darasa hilo lisilo na paa, alisema hawako salama kiafya.

Alisema afya ya akili na mwili wa mtoto huandaliwa akiwa ana umri wa kuanzia miaka sifuri hadi minane, hivyo kitendo cha watoto hao kuanza kukumbana na changamoto hizo, kinawaathiri kisaikolojia na hata ufaulu wao wa kimasomo.

"Katika eneo la muhimu kwa malezi ya mtoto ni umri huu ni vyema hata mzazi auze mifugo yake ili kuhakikisha mtoto anakuwa na msingi mzuri kuliko kuuza mali wakati mtoto ambaye tayari ameharibikiwa akiwa mdogo ili umpeleke sekondari," alisema Elphas.

Alisema shule ilipaswa kutambua athari za mazingira hayo kwa watoto wadogo. Wanafunzi wa madarasa ya juu ndiyo wasome humo badala ya wadogo zao wa darasa la awali na la kwanza.



Aliyekuwa Mkuu wa wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, Dk. Vincent Mashinji (kulia), akikabidhi nyaraka kwa Mkuu mpya wa wilaya hiyo, Kemirembe Lwota, wakati wa makabidhiano ya ofisi, mjini Mugumu juzi. Dk. Mashinji, amehamishwa na kuwa Mkuu wa wilaya ya Manyoni, mkoani Singida. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahamiaji haramu kutumikia kifungo miezi mitatu gerezani

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Tabora imewahukumu raia watatu wa Burundi kutumikia kifungo cha miezi mitatu gerezani au kulipa faini ya Sh. 500,000 kila mmoja baada ya kutiwa hatiani kwa kuingia nchini bila vibali.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mwandamizi John Mdoe, aliyesema kuwa, raia hao wa Burundi walikamatwa Julai 16 mwaka huu huko Ipuli Mnadani, mjini Tabora.

Alisema adhabu hiyo imetolewa na mahakama hiyo chini ya kifungu cha Sheria ya Uhamiaji Na. 45. Waliohukumiwa ni Paskali, Pasco na Mikulo Zambim, huku wote wakikiri kuingia nchini bila kibali chochote.

Baada ya hukumu hiyo, raia hao wa Burundi walikosa fedha hizo na kupelekwa gerezani kutumikia kifungo hicho cha miezi mitatu.

# Vigogo wa Ushirika wafikishwa kortini kwa tuhuma za rushwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga imewafikisha mahakamani viongozi wanane wa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) Kangeme na Mshindi, akiwamo Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Abdul Mauga, kwa tuhuma za rushwa.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga, Donasian Kessy, alieleza hayo juzi wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari hapa mjini kuhusu utekelezaji wa shughuli zao kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu.

Alisema walifikia hatua hiyo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wakulima wa tumbaku kwamba wamekuwa wakikosa malipo yao baada ya kuuza zao hilo kisha kuanza uchunguzi na kubaini kuwapo mianya ya rushwa.

Alisema vyama vilivyobainika kuwa na madeni ya wakulima ni 13, madeni hayo yakisababishwa na viongozi kutoa fedha katika akaunti za chama na kuzigawa kupitia akaunti zao binafsi.


"Tulichobaini kingine ni kughushi nyaraka na kufanya malipo yasiyo halali, kutoa fedha katika AMCOS na kuzitumia kwa matumizi yao binafsi.

"Baada ya kufanyia kazi malalamiko hayo, TAKUKURU tuliwafikisha mahakamani viongozi hao, akiwamo Meneja wa KACU, Abdul Ally Mauga kwa makosa ya kujihusisha na vitendo vya rushwa," alisema Kessy.

Alisema taasisi hiyo inaendelea kufanyia kazi malalamiko ya wanachama wengine wa AMCOS kutoka vyama 11 na kuhakikisha hatua stahiki zinachukukiliwa kwa viongozi wote waliojihusisha na vitendo vya rushwa.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema kuwa katika kipindi hicho walipokea malalamiko 46. Kati yake, 28 yanahusiana na rushwa na 18 yasiyohusiana na rushwa. Kesi zilizoko mahakamani ni 17.

Ukurasa 12



Uwekezaji kurudisha miti asili nyenzo inayobadili maisha ya watu na vijiji



**CCM mnadeni kwa Kinana, mpeni kumbukumbu**

Ukurasa 13



# Uzinduzi SGR mtaji unaomng'arisha Rais Samia nje, ndani ya mipaka

## •Bwawa Mwalimu Nyerere bandari kumpaisha zaidi

**Na Peter Orwa**

TANGU aingie madarakani, leo akihesabu safari zake kusonga miaka mitatu na nusu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa na staili mbalimbali za kuboresha uchumi na biashara katika zama za awamu ya sita.

Staili hiyo inabebwa na kunadi uchumi wa kuuza kilichomo sokoni Tanzania. Mathalani, alipoanza na tamthilia ya kuuza bidhaa utalii, pia anahamasisha uzalishaji na kukaribisha wawekezaj ambao ni muhimu kuwezesha kwa mitaji, teknolojia na hata masoko.

Ili kunakishi mikakati yake hiyo, mara moja akajitosa katika vita na ushawishi wa siasa uchumi kung'arisha nchi kwa marafiki wa uwekezaji mitaji ya kimataifa.

Pia, hapo ndipo ukawa mwanzo wa kushuhudiwa mengi yanayotafsiriwa kama maridhiano ya kisiasa na kufunguliwa vizimba vya mikutano ya kisiasa kitaifa.

Lingine ni kwamba, amekuwa akipambana tangu mwanzo wa utawala wake akiwekeza katika mitaji yake mikuu inayowezesha uchumi, miradi mikubwa ikiwamo Bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere na reli kipenzi cha Watanzania SGR na kulitekeleza hilo jana amezindua SGR.

Ili kufanikisha malengo yake katika mazingira ya dunia ambayo sasa ina sura ya kijiji, Rais amekuwa akizuru katika mataifa tofauti akitumia ushawishi kunasa vile ambavyo uwezo wake haumo nchini.

Baadhi ya matunda sasa yanaonekana katika nyendo kama uwekezaji



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa akinadi uchumi wake nchini Norway. **PICHA: IKULU**

ikiwamo katika sekta kama kilimo, mitaji na hata masoko ya bidhaa zake kama kunavyoshuhudiwa katika mazao ufuta na rasilimali mbolea, huku nyumbani rasilimali vijana ikiingizwa shambani kupata ajira katika teknolojia ya kisasa.

Nyumbani nako kunatumika msukumo uliopata kampeni za kiuchumi mwaka1964 maarufu "It Can Be Done, Play Your Part' kwa maana "inawezekana, timiza wajibu wako' kila sekta ilipambaniwa kufikia hatua zaidi ya maendeleo.

Ikirejewa katika ziara yake nchini Norway, Februari mwaka huu, mkuu huyo wa nchi anayeingia katika rekodi ya Rais wanawake duniani, akaitamkia hadhira iliyosikia hotuba yake kwamba, mwaka huu Shirika la Fedha Duniani (IMF), limesema "Tanzania inatarajia kuwa kati ya nchi 20 zenye uchumi unaokuwa kwa kasi duniani."

Rais Dk. Samia akibeba ajenda yake ya ushawishi mitaji, fursa za masoko na uzalishaji kuegemea nchini kwake, akawataka wawekezaji wa Norway kuja nchini Tanzania, kwani kuna mazingira mazuri ya kisiasa, kijiografia na kiuchumi.

Iikuwa jijini Olso, akihutubia mkutano wa Jukwaa la Biashara kati ya nchi hizo mbili, Rais Samia akabainisha kwamba tayari zipo kampuni kadhaa za Norway zilizotumia fursa hiyo vizuri kwa uchumi wa Tanzania.

Aidha, Dk.Samia akawaambia kwamba:"Tanzania ina amani chini ya demokrasia imara ya mfumo wa vyama vingi, unaozingatia tunu za utawala bora, kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria."

Ni hoja ambayo akaiunganisha na faida za kijiografia, akiwashawishi wawekzaji wa nchi hiyo na wengineo kuchagua Tanzania kuwekeza, kwani ina Bandari ya Dar es Salaam katika Bahari ya Hindi, inayohudumia mataifa manane ya Afrika inayopakana nayo.

Hata hivyo, bado tunu ya bandari ina muskatakabali mpana, hadi sasa kukiwapo nyingine baharini Mtwara, Tanga na bandari ndogo Bagamoyo, pia nyingine nyingi za katika maziwa mbalimbali nchini zikiendelea kufanyiwa maboresho makubwa.

Rais akatetea sera za uchumi wa nchi kwamba, ni imara na huku ukuaji wa pato la taifa (GDP) kwa sasa likiongezeka kwa kasi nzuri, asilimia 5.2 kwa mwaka, kukiwapo matarajio kufika aslimia sita kipindi kijacho, baada ya kuondokana na misukosuko ya maradhi ya COVID 19 duniani.

Rais Dk. Samia, akawasistiza wawekezaji wa Norway na serikali yao, kwamba kuna fursa tano za kupewa kipaumbele, akizitaja kuwa ni: kilimo, nishati mbadala, mafuta na gesi, mifuko ya uwekezaji, miundombinu na usafirishaji.

Ni aina ya uwekezaji ambao Rais Dk. Samia kwa kuzungika na maudhui kama hayo, amekuwa akisambaza hoja yake katika nchi mbalimbali duniani, ziungane kitaifa kukuza uchumi unaopiganiwa sasa na serikali.

**SGR, BWAWA NYERERE**

Mbali na kuwapo mazingira wezeshi ya kwa kunufaisha siasa uchumi, miradi miwili mikubwa ya kiatifa inayotelezwa sasa, ina tafsiri pana katika kasi ya ukuaji uchumi wa nchi na ushawishi wa uwekezaji kimataifa, ikiunganishwa na pacha wao bandari za nchini.

Msingi wa rasilimali nishati inavyojitosheleza kitaifa, daima inatoa tafsiri pana katika hatua ya uchumi wa nchi, samambaba na 'binamu yake' miundombinu ya usafiri.

Ikianzia na mvuto katika Afrika Msharikі, mathalan maboresho ya bandari iiyoko mkoani Rukwa na barabara zake, tayari imeleta mvuto mkubwa na soko bandari ya Dar es Salama, ambayo sasa inaunganishwa moja kwa moja na nchi jirani kama Zambia, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Congo (DRC).

Hatua ya kizinduliwa usafiri wa treni kwa reli ya SGR, pia mtambo mwingine wa umeme katika Bwawa la Umeme a Mwalimu Nyerere, kuwashwa hivi karibuni, kunabeba maana kubwa katika maendeleo ya uwekezaji wa 'Tanzania mpya yenye uchumi unaokua wa kasi' kwa wa mujibu wa IMF.

Tafasiri hiyo kiuchumi na siasa, inachangia kasi ya uchumi kuua kwa kasi nchini na kimataifa,uchumi unang'ara kukaribisha mitaji ya mbali, kama alikokuwa nchini Norway.

Ni changamoto sasa kwa watendaji wa kiserikali kuendelea alikoishia Rais katika jitihada zake, katika kukamilisha maendeleo ya uchumi wa taifa.

Simulizi ya maboresho ya kimfumo na kimtaji inapaswa kufungua nja zaidi, mathalani viwanda vipya vinavyowekezwa kuwa chanzo cha hatua zaidi.

UCHUMI

# Uwekezaji kurudisha miti asili nyenzo inayobadili maisha ya watu na vijiji

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Maliasili na Utalii, inatahadharisha kuwa kila mwaka zaidi ya hekta 400,000 za miti ya asili zinapotea zikikatwa kupata ardhi ya kujenga au kulima, mbao, kuni na mkaa.

Kukata miti hiyo muhimu inayopunguza athari za mabadiliko ya tabianchi si jambo jema kwani ni kuondoa 'mapafu' yanayofyonza hewa ukaa na kupunguza joto duniani.

Lakini jambo kubwa ni nani anayerudisha miti hiyo mamilioni inayokatwa kila uchao? Juhudi za kunusuru isikatwe zaidi zinachukuliwa na wadau wanaookoa mazingira, ikiwamo kampuni Udizungwa Corridor Limited inayoendeleza kazi hiyo wilayani Kilolo mkoani Iringa.

Uongozi wa kampuni hiyo umeingia makubaliano na vijiji vya Itonya, Mhanga na Uluti ili kuzuia ukataji miti hovyo wakati miti mipya inapopandwa.

Katika makubaliano hayo wananchi ndiyo wanaopanda miti na kusimamia ukuaji wake kwa lengo la kuendeleza maisha ya bayoanuai zote watu, wanyama na mimea.

Hans Kadinda (22) anayeishi kijiji cha Itonya wilaya ya Kilolo ni mwenye matumaini ya kuwa uwekezaji huo unalinda mazingira na kuboresha maisha ya wengine na ataweza kuwa na maisha bora kwake na mkewe na mtoto wao.

Akiwa mmoja wa wafanyakazi 150 wa kampuni ya Udizungwa Corridor, tangu mwaka 2021, anasema kuwa na kesho iliyobora ni hakika kwa upande wake kwa sababu uwekezaji kwenye miti umeangalia pia maisha bora kwa vijana na wanavijiji.

Japo hakuendelea na masomo ya sekondari kutokana na hali duni ya familia , Kadinda anajiunga na akifanyakazi ya upishi katika kambi ya kampuni hiyo iliyopo kijijini Mhanga inayo jishughulisha na kupanda miti.

Pamoja na kazi hiyo anamiliki pikipiki na amemfungulia duka mzazi mwenzake kijijini Mhanga ili kumwezesha kimapato.

Kadinda ni mmoja ya vijana wazawa wa wilaya ya Kilolo ambao wameajiriwa na UCL kampuni ambayo imewekeza kwenye mradi wa kupanda miti ya asili katika milima ya Udizungwa.

Miti mingi ya asili katika milima hiyo iliyopo kwenye ukanda wa Tao la Mshariki ilikatwa na wanavijiji na hata wageni kwa ajili ya matumizi mbalimbali na kama wataalamu wa msitu wanavyosema kila mwaka zaidi ya hekta 400,000 za miti ya asili hukatwa nayo pia ilitumbukia kwenye janga hilo.

Mtendaji wa kijiji cha Uluti, Zainabu Usama, anasema ujio wa kampuni hiyo umezuia ukataji haramu wa miti ya asili kutengeneza mkaa, mbao na kuni kwa matumizi ya nyumbani.



Baadhi ya wafanyakazi wakipanda miti ya asili shambani katika milima ya Udzungwa wilayani Kilolo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Anaongeza kuwa pamoja na ajira zilizopatikana, kijiji chake pia kimeweza kushuhudia biashara nyingi kama bodaboda, maduka na minada zikiongezeka kutokana na ongezeko la mzunguko wa pesa.

"Malipo ikiwamo mishahara, inaongeza mzunguko wa fedha kwenye minada na biashara nyingine . Vitu mbalimbali vinanunuliwa katika kijiji cha Mhanga kwenye ofisi na kambi ya UCL na pote kwenye kuuza na kununua." Anasema.

Zainabu anasema wafanyabiashara wanatoka sehemu mbalimbali kama vile makao makuu ya wilaya Kilolo kuja kuuza bidhaa zao na yote yamekuza biashara na uwekezaji.

Mtendaji huyo wa kijiji ambaye ni msomi wa chuo kikuu huria, anasema uwepo wa shughuli za kupanda miti unakinufaisha kijiji hicho kwani kinapokea Sh. milioni 10 kila mwaka kama fidia ya kutunza misitu asilia inayonyonya hewa ukaa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Uluti, Aidan Mmewa anaungana na Zainabu akiongeza kwamba tangu mwaka 2021, kumekuwepo na ongezeko la maendeleo mfano nyumba za bati kijijini hapo zimeongezeka.

Mumewe anasema ongezeko la watu katika kijiji hicho kunatokana na wafanyakazi na vibarua wa UCL umechochea mzunguko wa pesa katika eneo hilo.

"Vijana wetu wanapata kipato kutokana na uwepo wa ongezeko la watu wanaofanya kazi ya kupanda na kutunza miti ya asili," anasema.

Anasema pamoja na kupokea mrahaba wa kutunza miti, kampuni hiyo inachangia maendeleo mfano, kukamilisha majengo ya shule ya sekondari, vyoo vya Shule ya Msingi Mhanga na ofisi za kijiji chake.

Akizungumzia mafanikio ya kampuni ya Udzungwa, kwa kushirikiana na vijiji kadhaa wilayani Kilolo, Mkurugenzi Mkuu Fredrick Jailosi, anasema wameajiri zaidi ya wafanyakazi 150 na vibarua wengine wengi wanaofanya kazi kwa msimu kila mwaka.

"Wakati wa msimu wa kupanda miti kati ya mwezi Januari na Machi tunakuwa na vibarua zaidi ya 1,000 wanaofanya kazi kwa miezi sita kila mwaka," anasema Jailos.

Anaongeza kuwa kampuni inavilipa vijiji vinavyomiliki ardhi inayopandwa miti Shilingi 35,570 ambayo ni kodi ya pango kwa kila ekari moja kwa mwaka.

"Ardhi tunayolipia ni ile ambayo imeachwa baada ya kukatwa miti na sasa haina ubora wala thamani ya kufanya kilimo," anasema mkurugenzi huyo.

Anafafanua kuwa kampuni hiyo inayomilikiwa na Tanzania Forest Conservation Group na wakulima wadogo 174, ina malengo ya kupanda miti ya asili katika eneo la ekari 18,000.

Jailos anasema aina mbalimbali zaidi ya 100 za miti ya asili itapandwa wilayani humo kwa uwekezaji wa zaidi ya Sh. bilioni 90.

Alisema uwekezaji huo ambao ni wa muda mrefu mpaka mwaka 2051, unatarajiwa kuingiza mapato kupitia biashara ya hewa ukaa.

Mapato yatakayopatikana yatagawanya kwa ulinganifu yaani asilimia 50 kila mmoja kwa TFCG na wakulima wadogo ambao ni wanahisa.

"Lakini vijiji vitaendelea kupata malipo ya kila mwaka kama pango la ardhi na gharama za kutokata miti," mkurugenzi huyo anasisitiza.

Pango la ardhi la kila mwaka linatarajiwa kuongezeka kutoka 35,570 kwa ekari mwaka 2022 mpaka 68,000 itakapofika mwaka 2051 huku malipo ya hewa ukaa yatafikia bilioni 8.7 kwa mwaka.

Anasema vijiji pia vitapata malipo ya mavuno ya miti kwa ajili ya mbao na matumizi mengine kwa mujibu wa mkataba baina yao na mwekezaji.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## CCM mnadeni kwa Kinana, mpeni kumbukumbu




KUNA upepo fulani hivi umepita ndani ya CCM, chama tawala chenye umri wa miaka 47 ya kuzaliwa, lakini 70 ya kuona dunia, ikizingatiwa kuwa kilitokana na muungano wa Tanganyika African National Union (TANU) na Afro Shiraz Party (ASP) ya Zanzibar.

Upepo huo umetikisa matawi ya miti iliyooteshwa ndani ya chama hicho, baada ya aliyekuwa Makamu Mwenyekiti , komredi Abdulrahman Kinana, kuamua kujiuzulu uongozi lakini kuendelea kubaki ndani ya chama hicho.

Ni nadra sana kiongozi hususan wa Tanzania kujiuzulu bila kutenguliwa nafasi yake maarufu kama kutumbuliwa, sijui inatokana na nini, lakini inawezekana kila mtu ana wazo lake katika hilo, ila itoshe tu kusema inahitaji roho ngumu.

Ni wachache sana katika historia ya nchi hii, walioamua kuachia ngazi wenyewe na kukaa pembeni licha ya nafasi nzuri walizokuwanazo, akumbukwe Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye mwaka 1985 aliachia urais akisema anang'atuka.

Lakini pia aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Ali Hassan Mwinyi aliyefanya hivyo mwaka 1977 mwezi mmoja tu kabla ya kuzaliwa CCM, akiguswa na mauaji ya vikongwe yaliyotokea Shinyanga.

Hebu nambieni ni nani aliye tayari kujiuzulu leo kwa matukio yaliyofanywa na watu wengine tena mkoani? Nani? Watu wanang'ang'ania madarakani mpaka wang'olewe, hata kama wamebainika kuwa na hatia katika masuala mbalimbali.

Kujiuluzu kwa ndugu Kinana, hakika kumesababisha mjadala mpana sana huku watu wakijiuliza nani atachukua nafasi yake ndani ya CCM, mjadala umegusa wana CCM, wananchi wa kawaida na hata wapinzani ambao wengine kwa vyovyote wanachekelea jino pembe.

Hakika Komredi Kinana amefanya mambo mengi katika medani ya siasa nchini, akijulikana zaidi pale alipokuwa na umri wa miaka 44 aliposimamia kampeni za ndugu Benjamin William Mkapa mpaka kuwa rais wa tatu wa taifa la Tanzania.



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

Alifanya hivyo tena miaka 10 baadaye na kuwezesha kuingia madarakani ndugu Jakaya Mrisho Kikwete na kuwa rais wa nne wa taifa hili, na akirudia mwaka 2015 alipomwezesha ndugu John Magufuli kuwa Rais wa awamu ya tano.

Ni nadra sana kwa mwanasiasa kufanya haya kwa miaka 30, akiwezesha wengine kukalia kilele cha taifa bila kuingiwa na inda, na badala yake kuendelea kuwasaidia kwa karibu kwa hali na vitendo, katika uongozi wao na kufanikisha nchi kutulia.

Ndugu Kinana angekuwa na uchu wa madaraka, nani angemzuia kuchukua fomu na hakika kufanya vizuri katika kinyang'anyiro hicho? Ila alitosheka na alichokuwa nacho na alipokuwa hivyo, akaendelea kusaidia chama chake kuongoza nchi.

Hivi sasa lazima chama kinabungua bongo kumpata mrithi wake, lakini kikumbuke na kuzingatia kuwa ndugu Kinana ana nyayo panana ndefu hivyo anavaa kiatu kipana na kirefu. Kwa maana hiyo atafutwe mtu atakayevaa viatu hivyo vikamtosha.

Kiongozi huyu amefanya mengi ndani na nje ya CCM na kuacha alama ambayo haitafutika, na bila shaka wana CCM watamuenzi kwa alichokifanya, ingawa naamini kamailivyo ada ya Watanzania, atasahaulika muda si mrefu.

Atasahaulika na kusubiri kukumbukwa siku atakayokuwa amemaliza mwendo wake duniani, na ndiko wengi hujitokeza ama kuonyesha ya ndani ya mioyo yetu au kuumia kwa dhati, kutokana na kuondolewa huko, lakini naomba hili lisitokee kwa Kinana.

Mimi niliyepata kufanya naye kazi ndani ya chama hicho, nakumbuka siku aliponiita ofisini kwake na baada ya mazungumzo, akanikabidhi chupa ya mvinyo akiniambia ilimpendeza kunipa, ingawa alikuwa amepelekewa yeye kama zawadi ya Krismasi. Ilinifanya kujisikia vizuri sana na kumshukuru.

Hivyo basi kwa sifa hizi na zingine, CCM ina jukumu kubwa la kumkumbuka na kumwekea alama itakayodumu milele, hata kwa vizazi vijavyo, kwamba alipata kuishi mtu anaitwa ndugu Abdulrahman Kinana ndani ya CCM na Tanzania.

Wana CCM siku anatangazwa mrithi wake, natarajia mtamke kuwa moja ya viwanja vya michezo nchini mnavyovimiliki, kitaitwa kwa jina la 'Uwanja wa Abdulrahman Kinana'. Viwe Jamhuri Morogoro au Dodoma au iwe Mkwakwani wa Tanga. Kuna sababu gani ya kuwa na Jamhuri mbili? Mbona Liti iliwezekana? Hongera sana komredi Kinana.

BIASHARA

## MSHIKAMANO CHINA/AFRIKA

# Ushirikiano unavyojitokeza idara zote kibiashara, lugha, teknolojia na kisiasa

**Na Yi Xim, BEIJING**



Reli ya umeme - SGR ya Ethio-Djibouti iliyojengwa na China kuunganisha mataifa hayo. **PICHA: MTANDAO**

UHUSIANO kati ya nchi na watu wa China na Afrika unazidi kuimarika enzi hizi za maendeleo ya viwanda na teknolojia, ukilenga kuwaleta karibu na kuwaunganisha.

Tukirejea karibu karne nzima nyuma tunaona kuwa, treni ya mwendokasi kuelekea kwenye mafanikio, ilianza na Osman, mmoja wa wanafunzi 24 wa kwanza waliojiandikisha katika karakana ya Luban iliyoko nchini Djibouti.

Tangu utoto alikuwa na ndoto ya kuwa mfanyakazi wa reli na kwamba karakana ya Luban ilisaidia ndoto ya Osman kutimia. Ikijengwa mwaka 2019, inatoa programu ya miaka mitatu ikijumuisha masomo kwa nadharia na mazoezi ya uhandisi.

Baada ya kuhitimu, Osman alikuwa mfanyakazi mwanafunzi katika reli ya Addis Ababa-Djibouti, ambayo ni ya kwanza ya umeme iliyojengwa na China barani Afrika.

China ilitangaza kwa mara ya kwanza mpango wa kuanzisha karakana za Luban barani Afrika mwaka 2018. Karakana hizo zimepewa jina la mvumbuzi wa kale wa Kichina Lu Ban (kipindi cha majira ya masika na vuli, 770-476 kabla ya Masiha Yesu Kristo), ambaye alisifika kwa werevu na ufundi wake.

Ni takriban miaka 2,500 baadaye, karakana za Luban tayari zimekuwa chapa ya elimu ya ufundi ya Kichina barani Afrika.

Kama msemo wa zamani unavyosema, "mpe mtu samaki na umlishe kwa siku moja, lakini mfundishe kuvua samaki na umlishe maisha yake yote."

Karakana 11 za Luban zimeanzishwa katika nchi 10 za Kiafrika, zikitoa kozi zilizowekwa ili kukidhi mahitaji yao ya maendeleo. Hadi sasa, karakana za Luban zinatoa zaidi ya taaluma 70 katika maeneo kama vile roboti za viwandani, utoaji wa huduma za komputa na teknolojia ya habari mtandaoni, usimamizi wa usafirishaji na utunzaji wa shehena, dawa za asili na jadi za Kichina, biashara ya mtandaoni ya mipakani na kilimo cha kisasa.

Mafunzo hayo ya kitaaluma yamewapa maelfu ya vijana wa Kiafrika kama vile Osman wenye ujuzi na ustadi unaofaa kwa dunia inayobadilika kwa kasi, kuwapeleka kwenye treni ya haraka ya ushirikiano kati ya China na Afrika, sio tu kama abiria, lakini kama wahandisi na madereva wenye sifa ambao wanaweza kujipatia maslahi kwa maisha sasa na ya baadaye.

### LUGHA MOJA

Rais wa kwanza Mwafrika wa Afrika Kusini, Nelson Mandela, aliwahi kusema, "ukizungumza na mtu katika lugha anayoielewa, hiyo inaingia kichwani mwake. Lakini ukizungumza naye katika lugha yake aliyozaliwa nayo inaingia moyoni mwake."

Katika miaka ya hivi karibuni, kadri uwekezaji wa China barani Afrika unavyokua, ndivyo na mvuto wa lugha ya Kichina katika bara zima unavyokua.

Asha Fum Khamis ni mwalimu wa Kichina kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuanzia 2010 hadi 2013, amefundisha Kichina wanafunzi 300 wa Tanzania.

Anasema karibu wanafunzi 50 kati yao baadaye wamekuwa walimu wa Kichina pia.

Kadiri ushirikiano wa China na Afrika unavyozidi kuimarika katika nyanja mbalimbali, elimu ya China inazidi kuwa maarufu miongoni mwa vijana wa Afrika katika kutafuta fursa za maendeleo. Mandarin au Kichina kinazidi kuingizwa katika mitaala ya shule ya Kiafrika.

Mbali na wanafunzi wa Kiafrika wanaojifunza Kichina, vyuo vikuu vingi zaidi vya Kichina vinatoa kozi za lugha za Kiafrika, kuanzia Kizulu, Kiswahili, Kiamhariki, Kimalagasi hadi Kisomali na Kitswana, zaidi ya lugha 20 za Kiafrika sasa zinafundishwa katika vyuo vikuu vya Kichina.

Ushirikiano huo unajenga daraja la utamaduni na urafiki miongoni mwa vizazi vichanga na vya sasa na kuendelea kukuza biashara na ushirikiano.

Kuna methali moja ya Kichina inasemayo, "Kujifunza lugha ya kigeni ni kuwa na dirisha zaidi la kutazama ulimwengu." Kwa kujifunza lugha za kila mmoja, uhusiano wa kitamaduni na lugha kati ya China na Afrika umeimarika na mioyo ya watu hao wawili inakaribiana.

### SHEREHE KITAMADUNI

"Ndoto yangu ni yako. Ndoto yako ni yangu. Unataka furaha nami pia. Sote tuko sawa." Hili ni shairi la ujumbe wa wimbo wa filamu halisi ya Waafrika nchini China.

Ni filamu kuhusu simulizi za Waafrika wanaoishi na kufanya kazi nchini humo iliyotayarishwa kwa pamoja na wakurugenzi wa Kichina na Kiafrika.

Mwangwi katika hisia za ubinadamu huweka msingi wa kubadilishana kitamaduni. Katika miaka ya hivi karibuni, nchi nyingi zaidi za Kiafrika zinatoa majukwaa ya vipindi vya runinga na filamu za Kichina kufanya matangazo yake ya kwanza. Kutoka Memories of Peking, kipindi cha televisheni ambacho kimeenea sana nchini Nigeria na Côte d'Ivoire, hadi Operesheni Red Sea, wimbo wa Kichina ambao ulirekodiwa katika jangwa la Morocco, ushirikiano unaoshamiri wa filamu na televisheni kati ya China na Afrika unasimulia hadithi za China na Afrika katika zama mpya.

Historia ndefu na uhusiano wa kitamaduni kati ya China na Afrika pia hutoa msukumo mzuri kwa kutengeneza wa filamu. Tamthilia ya televisheni Karibu Milele ilitokana na hadithi za kweli za vizazi vya madaktari wa China walioko Afrika, ikijumuisha changamoto na matatizo waliyokumbana nayo na jinsi walivyoshirikiana na wenyeji hatua kwa hatua. Filamu hiyo ilichukuliwa katika maeneo sita kote China na Tanzania na hivi karibuni utaonyeshwa barani Afrika.

Afrika, kuna neno "Ubuntu," ambalo linaamini katika dhana ya kushirikiana ambayo inaunganisha binadamu wote. Ustaarabu wa Kichina pia unatetea wazo la maelewano na hisia ya jamii. Mfanano huo wa kitamaduni ndio chanzo cha nguvu ya China na Afrika kuimarisha urafiki na ushirikiano. Tunawatakia vijana wa China na Afrika kuungana mikono, mustakabali mwema kwa China na Afrika.



# Weledi, ubora watakiwa kwa mawakili wa serikali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Balozi Prof. Kennedy Gastorn, amewaagiza mawakili wa serikali kutekeleza falsafa ya Ofisi ya Mwansheria Mkuu wa Serikali (AG) ya kufanya kazi kwa kuzingatia weledi na ubora.

Prof. Gastorn alibainisha hayo jana jijini hapa, wakati akifungua kikao kazi baina ya ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali na wakurugenzi wa divisheni na wakuu wa vitengo vya sheria kutoka taasisi mbalimbali za serikali nchini.

Alisema mawakili wa serikali wanao wajibu wa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ubora, kwa kushirikiana na vyombo vingine kusaidia wananchi kupata haki yao.

"Falsafa ya ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali ni kutekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia weledi na ubora kujitambua na kutekeleza wajibu wetu kwa mujibu wa sheria,miongozo na taratibu,"alisema.

Akizungumzia kuhusu kikao kazi hicho alisema kimehusisha mawakili wa serikali kutoka mikoa pamoja na halmashauri zote Tanzania Bara.

"Kikao kazi hiki pamoja na mambo mengine kimekuwa na lengo la kuhakikisha miongozo ya utendaji inawafikia mawakili kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali, ikiwemo utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria iliyozinduliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi,"alisema.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, George Mandepo, alisema jukumu la la tume hiyo ni kupitia sheria zote, ili kubaini mapungufu na kupendekeza marekebisho na kutungwa kwa sheria mpya.

"Wizara, idara zimeanzishwa chini ya sheria fulani hivyo kabla ya kutoa mapendekezo ya kubadilishwa kwa sheria, lazima tuangalie kwanza wakati inaanzishwa wakati wa kati na wakati wa sasa ili tuweze kushauri kufanyiwa marekebisho yatakayo boresha sheria husika,"alisema Mandepo.

Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njohole, alisema kikao kazi hicho kitasaidia mawakili wa serikali kuzugumza lugha moja katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

"Mikutano kama hii inatusaidia mawakili kuzungumza lugha moja katika kutekeleza majukumu yetu ya kuhudumia wananchi hasa kwenye utoaji wa huduma za msaada wa kisheri kwa wananchi wetu kama ilivyo azma ya Rais wetu Samia Suluhu Hasan,"alisema.




Kamishna wa Idara ya uendelezaji Sekta ya Fedha katika Wizara ya Fedha, Dk. Charles Mwamwaja (katikati), akizungumza wakati akizindua kikundi cha Wakili Welfare Mkoba, jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Rais wa Tanganyika Law Society (TLS) Wakili Harold Sungusia na Mwenyekiti wa kikundi hicho, Wakili Laetitian Tagazwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TAKUKURU yataka ushirikiano kukabili rushwa kwenye uchaguzi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Singida imewataka viongozi wa dini, vyama vya siasa na mashirika yasiyo ya kiserikali kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo, ili kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha uchaguzi kufanyika bila kuwepo na mazingira ya rushwa.

Naibu Kamanda wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Petro Horombe, alisema hayo jana wakati akifungua semina kwa viongozi wa dini, vyama vya siasa, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na waratibu wa uchaguzi kutoka halmashauri zote za mkoa huu.

"Kama mnavyofahamu nchi yetu tunaelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, sasa TAKUKURU kama mratibu wa mratibu wa kupambana na rushwa haiwezi kufanya mambo haya pekee bila ushirikiano inahitaji wadau muhimu katika jamii ili kukomesha rushwa," alisema.

Alisema TAKUKURU inatambua kuwa viongozi wa dini na wa vyama vya siasa ni wadau muhimu sana katika kuzuia na kupambana na rushwa hasa katika uchaguzi, ili vitendo vya rushwa ambavyo vimekuwa vikifanyika kipindi hiki viweze kukomeshwa.

"Tunatambua nafasi ya viongozi wa dini ni kubwa sana katika kutengeneza tabia za wananchi,tunatambua viongozi wa siasa ndio wamiliki wa wagombea kwa hiyo wana nafasi ya kuweka misingi mizuri kuepuka vitendo vya rushwa katika uchaguzi.

Horombe alisema katika kuhakikisha wananchi wana uelewa juu ya madhara ya rushwa imekuwa ikitoa semina na mikutano vijijini kuwaelimisha waepuke na vitendo vya rushwa vinavyodhorotesha maendeleo .

Ofisa wa TAKUKURU, Joseph John, akiwasilisha mada kuhusu athari za rushwa kwa jamii, alisema rushwa imekuwa tatizo sana kipindi cha uchaguzi ambapo mgombea akifika kijijini tu wananchi wanamkimbilia awape rushwa.

"Wakati wa uchaguzi wananchi huwa wanaamini kuwa mgonbea asiyetoa rushwa huyo hafai, inabidi tuondoe dhana hii ili kufanya uchaguzi ulio huru na haki usiohusisha vitendo vya rushwa," alisema.

# 'Watumiaji huduma za kifedha ni asilimia 21'

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

LICHA ya watoa huduma za kifedha nchini kuongezeka lakini watumiaji wa huduma hizo bado ni asilimia 21 tu.Imeelezwa.

Kamishna wa Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Dk. Charles Mwamwaja alisema hayo wakati wa hotuba yake kwenye hafla ya uzinduzi wa kikundi cha Wakili Welfare M-Koba uliofanyika Jijini hapa jana.

Dk. Mwamwaja alisema watoa huduma za kifedha hapa nchini wameongezeka, lakini watumiaji wa huduma hizo bado ni asilimia 21 tu.

"Pamoja na ongezeko hilo la watoa huduma hiyo tulifanya utafiti wetu mwaka 2023 na kubaini kuwa watumiaji wa huduma za kifedha hapa nchini ni asilimia 21 tu hivyo kuna umhimu wa elimu kuendelea kutolewa kwa wananchi, "alisema.

Kadhalika, alisema serikali imeweka utaratibu mzuri utoaji wa huduma za fedha nchini kwa kuweka sera, sheria na miongozo inayolinda watoa huduma hao na wateja.

Aidha, alisema kwa upande wa watoa huduma za kifedha wanasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) hivyo wamekuwa wakiongezeka kwa sababu utaratibu uliopo ni mzuri.

Aidha, aliwataka mawakili hao kubuni miradi ya uwekezaji ili kuongeza mapato ya mfuko wao huo walioanzisha.

Aliongeza kuwa vikundi vingi wamekuwa na utaratibu wa kuishia kusaidiana wakati wa matatizo na kusahau kuwekeza kwenye sehemu zitakazosaidia kukuza mitaji yao.

Alizitaja sehemu wanazoweza kuwekeza ni kwenye mabenki, mifuko ya uwekezaji na kwenye miradi iliyotathiminiwa kitaalamu.

Mwenyekiti wa Wakili Welfare M-Koba ,Wakili Laetitian Tagazwa alisema kikundi chao kilianzishwa Desemba 24, mwaka jana.

Tagazwa alisema lengo la kikundi hilo ni kuwasaidia mawakili wenzao wanapopata misiba na matatizo mbalimbali.

Alisema hadi kufikia juzi kikundi hicho kilikuwa na wanachama 305 na mtaji wao umefikia kiasi cha shilingi milioni 220 na wanaendelea kusajili wanachama wapya kwa sharti la mwanachama mpya kununua hisa.

Mwenyekiti huyo alitaja matatizo yanakikabili kikundi hicho kuwa ni ukosefu wa elimu ya kifedha na jengo la ofisi ambapo kwa sasa watumia ofisi za wakili mwenzao mkoani Dar es Salaam.

Aidha, alimwomba mgeni rasmi huyo kuwasaidia kutafuta kiwanja jijini Dodoma, ili kujenga jengo la kudumu litakalotumiwa na wanachama wa kikundi hicho.



# Mbaroni akighushi nyaraka za serikali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa Kata ya Maendeleo jijini Mbeya, Dismas Nziku, amekamatwa kwa tuhuma za kughushi nyaraka mbalimbali za serikali vikiwamo vyeti vya kuhitimu Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Mtuhumiwa alikamatwa Julai 29, mwaka huu na Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mbeya, akiwa katika duka la vifaa vya shule ambako alikuwa ameajiriwa.

Mtuhumiwa anadaiwa kutumia duka hilo kughushi nyaraka mbalimbali zikiwamo za kuwasaidia wageni kupata hati za kusafiria nje ya nchi na kupata huduma nyingine serikalini ikiwamo kuwapatia haki ya kushiriki chaguzi mbalimbali.

Nyaraka nyingine alizokutwa nazo ni pamoja na vyeti vitatu vya kuzaliwa vya kughushi, vyeti vitatu vya kuhitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), leseni moja ya kufungisha ndoa, mihuri sita ya taasisi mbalimbali za serikali, binafsi na za dini.

Ofisa Uhamiaji wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji, Filbert Ndege aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu shughuli mbalimbali za idara hiyo.

Akielezea tukio hilo, alisema binti mmoja ambaye alifika katika ofisi za uhamiaji akihitaji kupata hati ya kusafiria na ndipo katika ukaguzi wa nyaraka zake maofisa wa intelijensia walihisi kuwa cheti chake cha kuzaliwa kilikuwa siyo halali.

Alisema walipofuatilia walibaini kilikuwa cha kughushi na ndipo wakashirikiana na maofisa wenzao wa kitengo cha ulinzi na udhibiti wa mipaka kufuatilia mpaka alikokitoa kitambulisho hicho.

"Walikwenda na binti huyo mpaka katika duka hilo la vifaa vya shule lililopo eneo la Sokomatola linalomilikiwa na Agnes Mhoka na huko ndiko walimkuta na nyaraka hizo ambazo amezitengeneza mwenyewe," alisema Kamishna Ndege.

Alisema nyaraka hizo ni hatari kwa usalama wa taifa kwa maelezo kuwa raia wa kigeni wanaopatiwa vyeti hivyo wanakuwa na haki ya kupata huduma zote za serikali kama ilivyo kwa Watanzania.

Vilevile, alisema watu hao wanaweza wakatumia nyaraka hizo kutekeleza matukio ya uhalifu nje ya nchi na wakaonekana kuwa ni raia wa Tanzania na hivyo wakachafua taswira ya nchi.

Aidha, aliwataka wananchi wanaohitaji huduma mbalimbali za idara ya uhamiaji kuhakikisha wanakwenda katika ofisi za jeshi hilo badala ya kuwafuata vishoka wa mitaani kwa maelezo kuwa watasababishiwa matatizo.

Hata hivyo, alimtaka mmiliki wa duka hilo kujisalimisha katika ofisi za idara hiyo kwa maelezo kuwa wakati wanafanya operesheni hiyo ya kumkamata kijana huyo yeye hakuwapo.

Mkuu wa Kitengo cha Ulinzi na Udhibiti wa Mipaka Mkoa wa Mbeya, Mrakibu wa Uhamiaji, Jerald Malidai, alisema wameshabaini kuwa kuna hilo wimbi la nyaraka nyingi za kughushi kutumika kwenye idara mbalimbali za serikali.

Alisema wataendelea kufanya ukaguzi kwenye maduka mbalimbali yaliyopatiwa uwakala wa kuwasaidia wananchi kufanya maombi kwa njia ya mitandao, ili kama wamiliki watabainika kuwa wanatumia mwanya huo kughushi nyaraka wachukuliwe hatua.

Aidha, alisisitiza kuwa watakaokamatwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (wapili kulia) akizungumza na Mkuu wa Idara ya Biashara za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo (katikati), baada ya uzinduzi wa maonyesho ya Kimataifa ya Wakulima ya Nanenane yanayofanyika kitaifa, katika viwanja vya Nanenane Nzuguni, jijini Dodoma jana. NMB ni miongoni mwa wadhamini wenza wa maonyesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Rungwe yajiwekea lengo kukusanya bilioni 7.4/-

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya imevuka lengo la ukusanyaji wa mapato kwa kufikisha Sh. bilioni 7.4 sawa na asilimia 120 ya Sh. bilioni 6.1 zilizopangwa kukusanywa mwaka wa fedha 2023/24.

Hatua hiyo imewafanya wadau kuishauri halmashauri kujiongezea malengo ya makusanyo ikidaiwa kuwa sio mara ya kwanza kuvuka malengo, kwa kuwa 2022/23 pia ilivuka kwa kukusanya zaidi ya Sh.bilioni 6.3 kati ya Sh. bilioni 6.1 iliyokuwa imejiwekea.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rungwe, Renatus Mchau, alisema mafanikio hayo ya ukusanyaji mapato yanatokana na sababu mbalimbali ikiwamo matumizi ya mfumo mpya wa ukusanyaji mapato wa Tausi ambao alisema unazuia wakusanyaji kuiba.

"Lakini tuna utaratibu wa semina elekezi za mara kwa mara kwa maofisa watendaji wa vijiji na kata, ugawaji wa pikipiki kwa kata zote 29, ili kukusanya mapato hususani maeneo ya vijijini na motisha za mara kwa mara kwa kata zinazofanya vizuri," alisema Mchau.

Akifungua kikao kazi na elekezi dhidi ya ukusanyaji wa mapato ya serikali, usimamizi wa miradi na sheria ndogondogo, usimamizi wa ardhi na mazingira kilichohudhuriwa na maofisa watendaji wa vijiji na kata zote, Mchau aliwapongeza wote waliofanikisha kufikisha mafanikio hayo ya makusanyo.

Aidha, aliwakumbusha watendaji wajibu wao katika kusimamia sheria, taratibu na kanuni mbalimbali, ili kuwaletea maendeleo wananchi na kuboresha utawala bora mambo aliyosema lazima pia yachagizwe na ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Aidha, alisema kila mtendaji ana wajibu wa kuhakikisha miradi ya maendeleo inasimamiwa ipasavyo, wananchi kushirikishwa katika kubuni na kuendeleza miradi, pamoja na kusikiliza kero za wananchi.

# Wananchi wataka barabara nzuri maeneo ya uwekezaji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imeombwa kufanya maboresho ya barabara kuelekea katika maeneo ya uwekezaji mkubwa pamoja na kuja na mfumo wa elimu kwa vitendo na ubunifu, ili kukubaliana na tatizo la ajira nchini.

Ombi hilo lilitolewa juzi na makundi tofauti ya wakazi wa Wilaya ya Njombe walioshiriki katika majadiliano kuhusu mpango wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya miaka 25 ijayo yaliyofanyika mjini hapa.

Mmoja wa wakazi wa Wilaya ya Njombe, Andrea Mahali alisema wilaya hiyo imepiga hatua katika sekta ya kilimo hivyo ni vizuri dira hiyo itazame katika kujikita kwenye kuboresha miundombinu ya barabara, ili kusiwe na kikwazo kwa wawekezaji.

Ally Mhagama alisema ili wilaya hiyo ipige hatua zaidi serikali inapaswa kuleta mfumo wa umwagiliaji, barabara za uhakika maeneo ya uzalishaji, kurekebisha sheria za kodi kwa wawekezaji wa viwanda pamoja na sekta ya elimu.

Pia alisema wanatamani kuona Watanzania wanakuwa na maadili kwenye nyanja zote jambo litakalosaidia kuwa na kizazi salama. Awali, wakieleza changamoto zilizokwamisha kasi ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2000-2025 Ofisa Mipango wa Halmashauri tatu zinazounda Wilaya ya Njombe akiwamo, Marco Balaga alisema kuna tatizo la kufikia mafanikio makubwa ya kiuchumi huku akitolea mfano Halmashauri ya Wilaya ya Njombe barabara ni za kiwango cha vumbi na hazipitiki kwa urahisi wakati wa masika hali inayosababisha kusuasua kwa shughuli za kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema tamanio lake ni kuona mpango huo wa Dira ya Taifa unakuja na suluhisho la matatizo kwa vijana.

"Dira yetu ya miaka 25 ijayo izingatie sana kuwapa fursa vijana sio tu ajira, kila fursa iwepo awepo kijana na kikianzishwa kiwanda kiwe na nafasi ya vijana," alisema Kasongwa.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Njombe, Justin Nusulupila, alisema dira hiyo itazame kwenye kilimo na miradi ya kimkakati ya madini ya chuma cha Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma eneo la Wilaya ya Ludewa.



# Kasi ukuaji miji inavyoua uoto, miti ya asili Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UOTO wa asili katika Visiwa vya Zanzibar umeendelea kupungua na kuelekea kupotea kwa miti na misitu kutokana na shughuli za kibinadamu ikiwamo ukuaji wa miji.

Aidha, ukuaji huo umesababisha ujenzi wa majengo kuchukua nafasi kubwa ya ardhi kwa kadri idadi ya watu inavyoongezeka huku mabadiliko ya tabia nchi yakipunguza ukubwa wa eneo husika.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Migombani Mjini Zanzibar kuhusu mpango wa kurithisha Zanzibar ya kijani.

Alisema katika kuendelea kutekeleza mikakati ya kuvinusuru Visiwa vya Zanzibar na kupunguza kasi ya athari za mabadiliko ya tabianchi inayoikumba dunia, serikali imeanzisha mpango wa kuirithisha Zanzibar ya kijani.

Aidha, alisema lengo ni kuweka uwajibikaji kwa kila mwananchi kupanda na kutunza miti ya misitu na matunda kwa ajili ya kuendeleza hali ya kijani Zanzibar. "Utekelezaji wa mpango huu wa urithi wa kijani utakuwa shirikishi kwa kuwaleta wadau wote pamoja kutoka sekta na ngazi zote. Mpango huu unakusudia kuongeza hamasa kwa kila mtu kushiriki kikamilifu na kujenga jamii yenye utamaduni endelevu wa kupenda, kupanda, kutunza na kutokata miti ovyo," alisema waziri huyo.

Aidha, alisema Zanzibar inafahamika kuwa ni visiwa vyenye mandhari ya kuvutia kutokana na kuwapo kwa aina tofauti ya miti ambayo inatoa haiba nzuri na kuifanya Zanzibar kuendelea kuwa ni visiwa vya viungo (spice island).

"Miti hiyo ndiyo inayofanya Zanzibar kuwa ya kijani na kuwa na bioanuwai za aina tofauti zinazotumika katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kimazingira, ikiwamo uhifadhi wa maji ya ardhini ambayo ndio chanzo kikubwa cha majisafi na salama kwa matumizi yote Zanzibar.

"Hali hii imetokana na uoto wa asili pamoja na juhudi mbalimbali zilizochukuliwa na serikali za awamu tofauti za kushajihisha jamii kupanda miti ya aina mbalimbali katika maeneo yao," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira, Sheha Mjaja Juma, alisema chimbuko la kuanzishwa mpango wa kurithisha Zanzibar ya kijani, inatokana na hali halisi iliyopo ya kuanza kupotea kwa miti ya misitu kunakopelekea kupungua kwa asili ya Zanzibar kuwa ya kijani. Alisema sensa ya mwisho ya msitu iliyofanyika mwaka 2012/2013 ambayo inaonesha kuwa uwezo wa misitu wa Zanzibar kutosheleza mahitaji ya ndani ni mdogo ambapo kwa wastani unamahitaji ya mita za ujazo 1,340,069 kwa mwaka.

"Uwezo wa uliopo wa misitu ya Zanzibar ni kuzalisha mita za ujazo 485,532 kwa mwaka sawa na asilimia 36 tu ya mahitaji. Wananchi wengi kwa sasa hawana utamaduni wa kupanda miti badala yake wanatumia mashamba ya urithi pasi na kuendeleza utamaduni uliofanywa na wazee wao wa kupanda miti," alisema.

Aidha, alisema hali hiyo imepelekea kupotea kwa bioanuwai, kuongezeka kwa mmong'onyoko wa udongo na hatimaye kupotea kwa haiba na hali ya kijani ya visiwa vya Zanzibar, kupungua kwa vyanzo vya maji na kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mpango wa kuirithisha Zanzibar ya kijani ni mpango shirikishi ambao utekelezaji wake utasaidia kuirejesha Zanzibar, kwenye asili ya visiwa vya kijani na kuimarisha urithi na utamaduni wa kupanda miti na kuitunza ambao utasaidia kuhifadhi mazingira.



Abiria wakining'inia kwenye gari lililo kwenye mwendo likitokea Mkoani kwenda Chake-chake, kisiwani Pemba jana, kitendo ambacho ni hatari na kinyume cha sheria za usalama barabarani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Rais ataka kasi ujenzi wa barabara

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amemtaka mkandarasi wa Kampuni ya Comfix & Engineering anayejenga Bandari ya Shumba Mjini Pemba kuhakikisha wanamaliza ujenzi kwa wakati uliopangwa kwa kiwango kilichokusudiwa na kushindwa kufanya hivyo atakuwa amejinyima fursa ya kuendelea kufanya kazi na Serikali ya Zanzibar.

Akikagua maendeleo ya ujenzi wa bandari hiyo jana Kisiwani Pemba, Hemed alisema eneo la Bandari ya Shumba lina uhitaji mkubwa kwa wananchi wanaoishi hapo hasa ukizingatia shughuli zao nyingi za kiuchumi zinategemea Bandari kwa kutoa na kupokea bidhaa kutoka nchi jirani.

Alisema kukamilika kwa bandari hiyo itatoa fursa ya kupatikana kwa ajira kwa vijana wazawa na wa vijiji jirani sambamba na kuwaondolea changamoto ya kusafiri masafa ya mbali kwa ajili ya kusafirisha na kupokea mizigo yao.

Makamu huyo alisema endapo Kampuni ya Comfix itashindwa kukamilisha mradi kwa wakati uliopangwa italazimika kuilipa, serikali kutokana na hasara watakayoisababishia kwa kipindi chote ambacho wamefanya kazi nje ya makubaliano ya kimkataba.

Wakati huo huo, Makamu wa Pili wa Rais alikagua ujenzi wa barabara ya Micheweni - Kiuyu Maziwang'mbe yenye urefu wa kilomita 7.5 inayojengwa na Mkandarasi Kampuni ya Iris Contraction Company inayotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi wa Septemba mwaka huu.

Alisema serikali imejipanga kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara zote zilizomo katika mpango mkakati mjini na vijijini, ili kuharakisha upatikanaji wa maendeleo kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Aidha, Hemed alimtaka mkandarasi Salim Construction Ltd, anayejenga mradi wa Shule za Sekondari Konde na Kifundi kuongeza kasi katika ujenzi wa mradi hiyo pamoja na kufanya kazi usiku na mchana, ili kuhakikisha wanakabidhi miradi hiyo kwa wakati uliopangwa.

Alisema dhamira ya Rais, Dk.Hussein Mwinyi ni kuona wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri yenye miundombinu bora inayokidhi mahitaji yote ya kufundishia na kujisomea, ili Zanzibar iwe na wasomi bora wa fani mbalimbali.

Aidha, aliwataka wananchi wa Jimbo la Konde kuacha kusikiliza maneno yasiyo na tija kwao na badala yake wamuunge mkono Rais Dk. Mwinyi katika kuhakikisha Taifa linasonga mbele kimaendeleo. Mawaziri wenye dhamana ya kusimamia miradi hiyo wamesema dhamira ya serikali ni kuhakikisha inawaletea maendelelo wananchi wake hivyo watahakikisha wanasimamia vyema miradi hiyo, ili kukamilika kwa wakati uliopangwa na ubora uliokusudiwa kwa lengo la kuwaondolea changamoto zinazowakabili wananchi wote wa Zanzibar.

Mawaziri hao ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa na Waziri wa Mawasiliano, Miundombinu na Usafirishaji, Dk. Khalid Salum Muhamed, walisema Rais Dk. Mwinyi ametekeleza kwa vitendo yale yote aliyoyaahidi kwa wananchi na ilivyoelekezwa katika ilani ya CCM.

# Jussa ataka uwanja wa ndege, bandari Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT -Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu, amesema Pemba haiwezi kufunguka kiuchumi bila kuwa na bandari ya kisasa na uwanja wa ndege wa kimataifa.

Aidha, amesema kukosekana kwa vitu hivyo ndio chimbuko la mfumko wa bidhaa kisiwani humo.

Jussa aliyasema hayo jana wakati akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika Uwanja wa Maziwa Ng'ombe Jimbo la Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema kukosekana kwa bandari ya kisasa kumesababisha makontena ya mizigo kushushwa katika Bandari ya Malindi Mjini Unguja na bidhaa kusafirishwa kwa gharama nyingine kisiwani Pemba, jambo lililoongeza gharama mara mbili kwa mfanyabiashara na kumuumiza mwananchi.

Alisema pamoja na serikali kuahidi kujenga bandari ya kisasa Kisiwani Pemba mwaka 2020 pamoja na uwanja wa ndege, lakini hakuna kilichofanyika mpaka sasa jambo ambalo linachangia kurejesha nyuma maendeleo ya kisiwa hicho.

Hata hivyo, alisema kwamba Uwanja wa Ndege wa Pemba na Barabara ya Mkoani hadi Chakechake, Kisauni hadi Fumba na Tunguu hadi Makunduchi zilikuwa zijengwe kupitia fedha za mkopo wa mfuko wa maendeleo wa Uingereza na kazi hiyo ilikuwa ifanywe na kampuni ya kizalendo ya Mecco lakini mradi huo umekwamishwa.

"Mradi wa uwanja wa ndege umeshatolewa fedha kupitia mkopo ambao umedhaminiwa na Serikali ya Muungano kwa mara ya kwanza haijawahi kutokea Euro milioni 457 (sawa na Sh. bilioni 1.3) zilikuwa zijenge uwanja wa ndege na barabara ya Chakechake/Mkoani, Tunguu /Makunduchi na Fumba hadi kisauni lakini ziliyeyuka," alisema Jussa.

Alisema kutokana na matatizo yaliojitokeza kampuni hiyo ya Mecco imelazimika kukimbilia mahakamani kwa sababu ilikuwa tayari imeshasaini mkataba wa mradi huo na ujenzi ulikuwa uwaze kufanyika Novemba mwaka jana.

Akizungumzia mradi wa ujenzi wa barabara ya Chakechake hadi Wete kuendelea kuzorota, alisema tatizo la chimbuko hilo ni serikali pamoja na wafadhili Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ) na mfuko wa Saud Fund.

Jussa alisema fedha za mradi huo zimekuwa hazipatikani kwa wakati na kulazimisha mkandarasi wa kampuni hiyo kukopa benki, ili kuhakikisha mradi huo utekelezaji wake unaendelea kufanyika.

Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, alisema Wilaya ya Micheweni Pemba inautajiri mkubwa lakini haujatumika ikiwamo ukubwa wa eneo la ardhi na kuwa na mazao mengi ya baharini jambo ambalo lingemaliza tatizo la umaskini kwa wananchi.

Aidha, alisema ripoti mbalimbali zinaonesha wilaya hiyo inakabiliwa na tatizo la umaskini na maradhi ikiwamo utapiamlo, lakini kama mipango ingetumika vizuri, umaskini ungeondoka kwa wananchi.

Kuhusu matumizi bora ya ardhi, aliwataka wananchi wa Micheweni kuwa makini na wawekezaji na kutoa mfano wananchi walivyoathirika na matatizo ya ardhi iki-

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**NEEMA .A. MSUYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 3093-0011** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KANANURA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2010. Kwa yeyote atakaekionaatoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/160205/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EVELINA ZEBEDAYO MNOBWE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3606-0051** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MASUMBWE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2022. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polis: **TB/RB/2850/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GERALD KOMBA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0938/0681** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MBEZI BEACH HIGH SCHOOL - KIRAMUU** mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **WH/RB/0429/16.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**VICTOR EMMANUEL MWEMEZI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.1599-0786** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BAOBAB SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/TPM/159809/2024.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENS. ACT.**
**(CAP.117 R.E.2002)**
**DEED POLL**



By this deed poll I the undersigned **DEBORA KENETH ASUMWISYE** formerly known as **DEBORA KENETH MELELE** do here by absolutely renounce and abandon the said name **DEBORA KENETH MELELE** and in the lieu there of assume the name as **DEBORA KENETH ASUMWISYE** and in pursuance of such change of name as afore said I hereby declare that I will be known at all time here in after in all actions and proceeding in dealings and transaction and upon all occasion what so ever use and sign name of **DEBORA KENETH ASUMWISYE** as my former name **DEBORA KENETH MELELE** renounce as afore said.
And I do here by authorize and request all person designate, describe and address me as where of I have into subscribe my old name **DEBORA KENETH MELELE** and the new name of **DEBORA KENETH ASUMWISYE.**
The reason for the change is that **DEBORA KENETH ASUMWISYE** is the name that appears in my all authorized documents.
**AND I HERE BY AUTHORIZE** and request all person to address me such assumed names instead of the names renounced.

**SIGNED** and **DELIVERED** by said **DEBORA KENETH ASUMWISYE** who is Known to me personally/~~identified to me by~~ ..........................................

In my presence this **19th Day of July, 2024**

DEPONENT

BEFORE ME:
NAME ..........
SIGNATURE ..........
ADDRESS ..........
QUILIFICATION ..........

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ORANDO JOHN KAMBARAGE** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 502 BDD na MC 448 BDH** aina ya **Fekon.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAN/MUH/7523/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MICHAEL ALOYCE MCHAKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye umiliki wa kampuni ya **TANZANIA CHINA TRADE AND TOURISM DEVELOPMENT LTD** yenye namba za usajili **MC 377 CRV – SINORAY.** CHASSIS NUMBER **LD3PCK6J7L2012295.** ENGINE NUMBER **SR162FMJ20092115.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/4765/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CLEMENT EMMANUEL NZELA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.456 ALD,** yenye Chassis No. **FUSU520612** na Engine No. **DC91AZF460** aina ya **MITSUBISHI FUSO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya Polisi.
**PHQ/SHI/KAH/6229/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CLASS CELL LIMITED** WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI **MC 102 ACZ** ILIYOPOTEA, KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/10795/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUSTINE MAKOMONDI KISUSI** anatangaza kupotea kadi ya gari aina ya **LANDROVER-DISCOVERY** yenye usajili namba **T 373 CAE,** CHASSIS NAMBA: **SALLTGM833A779885** na ENGINE NAMBA:**16P08007A.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/KIL/HAI/17525/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IMANI N ULOMI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T642 ABZ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/158164/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DICKSONI GERVAS KIMARIO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 323 EHT** aina ya **SHELOLAI.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DOD/KON/32282/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai Na. 94/2024**

**JINA LA MDAI .................................. FRIDA JOHN MAGANGA**

**JINA LA MDAIWA ............... DANIEL CHRISTOPHER SAGAYA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA**
**DANIEL CHRISTOPHER SAGAYA**
**S.L.P. 1657, DODOMA. 0626 355 742**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TSH. 15,000,000/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 06 mwezi 08 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 Mwezi 07 Mwaka 2024.

HAKIMU

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,
KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Kamala amkaba koo Trump

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, ameonekana kuwa mwiba kwa mpinzani wake Rais wa zamani, Donald Trump, baada ya kura ya maoni kuonyesha akiongoza katika majimbo tofauti ya nchi hiyo.

Harris ambaye anatafuta kuwania mgombea wa nafasi ya urais kupitia chama cha Democrat na Trump wapo katika mchuano mkali katika kupigania kuingia Ikulu ya White House katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Katika kura za maoni zolizotolewa juzi zinaonyesha Harris , ameziba pengo kati yake na Trump katika majimbo muhimu yanayotajwa kuwa yanatoa mshindi.

Harris yuko mbele katika majimbo manne muhimu, wakati rais huyo wa zamani yuko mbele katika mengine mawili, hayo ni kulingana na kura ya maoni iliyofanywa na Bloomberg News.

Makamu huyo wa rais yuko mbele dhidi ya Trump katika jimbo la Michigan kwa asilimia 11 na Arizona, Wisconsin na Nevada, anaongoza kwa pointi mbili.

Trump ana faida ya pointi nne katika jimbo la Pennsylvania na kuongoza kwa pointi mbili North Carolina, huku wawili hao wakifungana katika jimbo la Georgia.

Ikiwa matokeo ya kura ya maoni yangepigwa sasa, mgombea aliyeshinda Georgia angechaguliwa kuwa rais.

Katika kura ya maoni iliyoidhinishwa na Mfuko wa Maendeleo wa PAC, Harris anaongoza dhidi Trump kwa asilimia 48 hadi 47 huko Georgia, huku Trump akiwa mbele kwa alama mbili Arizona na Pennsylvania.

*Al Jazeera*



Kiongozi wa Iran, Ayatullah Ali Khamenei akiongoza sala mbele ya jeneza la Ismail Haniyeh na mlinzi wake mjini Tehran jana. **PICHA: ALLIANCE**

# Maelfu Iran waaga mwili wa Haniyeh

**TEHRAN,** IRAN

KIONGOZI Mkuu wa Iran, Ayatullah Ali Khamenei, jana ameongoza sala ya mazishi ya mkuu wa kisiasa wa kundi la Hamas, Ismail Haniyeh, aliyeuawa kwa shambulizi la angani.

Haniyeh aliuawa akiwa katika nyumba aliyofikia jijini Tehran, baada ya kuhudhuria sherehe ya kuapishwa kwa rais mpya wa Iran.

Khamenei aliongoza sala hiyo, kabla ya maiti ya Haniyeh kusafirishwa hadi nchini Qatar ambako anazikwa leo baada ya sala ya Ijumaa.

Maelfu ya waombolezaji walikusanyika katika chuo kikuu cha Tehran, wakiwa wamebeba mabango yenye picha za Haniyeh, huku wakipaza sauti za kuzilaani Israel na Marekani.

Televisheni ya taifa ya Iran, ilionyesha majeneza ya Haniyeh na mlinzi wake yakiwa yamefunikwa bendera ya Palestina wakati wa sala hiyo iliyohudhuriwa pia na maofisa wa ngazi za juu wa Iran, akiwamo Rais Masoud Pezeshkian na mkuu wa Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi, Jenerali Hussein Salami.

Kwenye sala hiyo, mkuu wa sera za nje wa Hamas, Khalil al-Hayya, aliapa kwamba ujumbe wa Haniyeh utaendelea kuishi na kwamba watakabiliana na Israel hadi watakapoing'oa kutoka kwenye ardhi ya Palestina.

Spika wa Bunge la Iran, Mohammad Bagher Ghalibaf, alisema kwamba nchi yake itatekeleza amri ya kiongozi mkuu Khamenei, akimaanisha kulipiza kisasi mauaji ya Haniyeh.

„Ni jukumu letu kujibu mauaji haya kwa wakati muafaka na mahala muafaka." Alisema spika huyo.

Mara tu baada ya mauaji hayo kutangazwa siku ya Jumatano, Ayatullah Khamenei alisema kwamba ulikuwa ni wajibu wa Iran kulipiza kisasi kwa damu ambayo imemwagwa ndani ya ardhi ya nchi yake.

Gazeti la New York Times liliwanukuu maofisa wa Iran wakisema kwamba kiongozi huyo aliamuru nchi yake kuishambulia moja kwa moja Israel.

„Mazayuni hivi karibuni watayashuhudia matokeo ya tendo lao la woga na la kigaidi." Alisema Rais Pezekshian, ambaye alikuwa kiongozi wa mwisho wa ngazi za juu wa Iran kukutana na Haniyeh siku ya Jumanne kabla ya kuuawa kwake.

Haniyeh alikuwa ziarani nchini Iran kuhudhuria kuapishwa kwa Pezekshian.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alisema mashambulizi hayo na yale ya Beirut, yaliyomuua kamanda mkuu wa kundi la Hizbullah, Fouad Shukr, yalikuwa"muendelezo wa hatari katika vita.01:43

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilikutana kwa dharura siku ya Jumatano kujadili tukio hilo kwa ombi la Iran.

Kwenye mazungumzo yao kwa njia ya simu, mawaziri wa mambo wa kigeni wa Misri na Jordan waliishutumu Israel kwa kuchochea hali kuwa mbaya zaidi.

Kwa upande wake, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alitoa wito kwa pande zote kujikita kwenye kukomesha mapigano.

Hata hivyo, Waziri Mkuu wa Qatar, Sheikh Mohammed bin Abdulrahman Al-Thani, alisema mauaji ya Haniyeh yameutia mashakani mchakato mzima wa kusaka makubaliano ya kusitisha mapigano.

Qatar inaongoza vikao vya majadiliano ya kusitisha mapigano, kwa upande wa Hamas ujumbe wake ulikuwa ukiongozwa na Haniyeh.

**DW**

# Maduro atishia kuwafunga wapinzani

**CARACAS,** VENEZUELA

WAKATI shinikizo la kimataifa likiendelea kupinga kuchaguliwa tena, rais wa Venezuela Nicolas Maduro, kiongozi huyo ametishia kuwafunga viongozi wawili wa upinzani.

Maduro alipa viongozi hao, Maria Corina Machado na Edmundo Gonzalez Urrutia, hawatayapata kamwe madaraka wanayoyataka.

Mrithi huyo wa kiongozi wa kisoshalisti na mtetezi wa sera ya Hugo Chávez, alitangazwa kuchaguliwa tena kwa muhula wa tatu hadi mwaka 2031.

Katika matokeo ya kura yaliyotangazwa Jumapili , Maduro alipata ushindi wa asilimia 51.2 ya kura dhidi ya Gonmzalez aliyepata 44.2.

Matokeo hayo yanayopingwa na nchi nyingi, huku wafuasi wa upinzani wakiendelea kuandamana kupinga matokeo ya uchaguzi.

Awali Maduro alitoa wito kwa wafuasi wake kujitokeza kwa wingi katika mitaa ya Caracas siku ya Jumatano, ili kuonyesha nguvu zake kwa upinzani.

Lakini maandamano hayo hayakufanikiwa kama yale ya wapinzani yaliyofanyika siku moja kabla, wengi waliojitokeza walikuwa wafanyakazi wa umma.

Mkuu wa diplomasia wa Marekani kwa nchi za Amerika ya Kusini, Brian Nichols, alitangaza mgombea wa upinzani nchini Venezuela, Edmundo Gonzalez Urrutia, ndiye mshindi.

Nichols alisema kwamba tofauti hiyo ya kura ilihesabiwa katika mamilioni ya kura na ikathibitisha ushindi usioweza kupingwa.

**RFI**

**Mrithi huyo wa kiongozi wa kisoshalisti na mtetezi wa sera ya Hugo Chávez, alitangazwa kuchaguliwa tena kwa muhula wa tatu hadi mwaka 2031.**

# AZAM SASA WAPO TAYARI KWA LIGI KUU, LIGI YA MABINGWA

Na Adam Fungamwango

KIKOSI cha Azam FC kilirejea jana asubuhi nchini kutoka kwenye kambi ya wiki tatu nchini Morocco, huku Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe, akisema wamepata maandalizi mazuri na kikosi chao sasa kipo tayari kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, Ibwe, alisema kwa kipindi chote walichokuwa huko wamefanya mazoezi pamoja na kucheza mechi za kirafiki ambazo zimewajenga kiasi cha kujua wapi pa kuanzia.

"Kambi ilivutia sana, sasa tunakwenda kwenye nyakati ambazo kila mtu atazifurahia, sasa tunaona tupo tayari, tumejiandaa vizuri, tuna timu nzuri na ya ushindani," alisema.

Ikiwa nchini Morocco, Azam ilicheza mechi tatu, ya kwanza dhidi ya US Yacoub Al Mansour na kushinda mabao 3-0, ikacheza dhidi ya Union Touarga Sport na kutoka sare ya bao 1-1, kabla ya kupata kipigo cha mabao 4-1 kutoka kwa Wydad Casablanca.

Akizungumzia mechi hiyo, Ibwe alisema ilikuwa ni mechi ambayo imewafundisha vitu vingine ambavyo wanatakiwa kwenda kukabiliana navyo katika mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunafurahi kucheza na timu kubwa ya Wydad Casablaca kwa sababu imetupa somo. Nilichojifunza, ukicheza na timu kubwa za aina ile, ukikosea tu mara moja basi ndiyo hapo hapo wanakuangamiza, maana ilikuwa kila tukifanya kosa tunaadhibiwa," alisema Ofisa Habari huyo.

Naye kiungo wa timu hiyo, Feisal Salum alisema mechi yao dhidi ya Wydad Casablanca ilikuwa ngumu na ilikuwa kipimo tosha kwao.

"Mchezo dhidi ya Wydad Casablamca umetuamsha na kujifunza vitu vingi, na inatutaka tuwe makini muda wote kwa sababu tunakwenda kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema.

Kikosi cha Azam kilitarajia kuondoka jana usiku kuelekea nchini Rwanda kwa ajili ya mechi ya kirafiki dhidi ya Rayon Sport kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kuzoea hali ya hewa, kwani itacheza dhidi ya APR ya huko huko katika mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Mashujaa FC yapania tano bora Ligi Kuu

Na Shufaa Lyimo

BENCHI la ufundi la timu ya Mashujaa FC limesema malengo yake ni kushika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, ili waweze kupata nafasi ya kushiriki mashindano ya Kimataifa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohamed Bares alisema kutokana na kikosi alichokisajili anaamini ndani ya msimu ana uhakika wa kutoa ushindani mkubwa.

"Malengo yangu ni kumaliza Ligi ndani ya tano bora msimu huu unaokuja na tumejipanga vizuri zaidi kama timu," alisema Bares.

Aidha alisema kuwa msimu ujao utakuwa na upinzani mkubwa kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu kipindi hiki cha maandalizi.

Aliongeza kuwa amebaini mapungufu machache kwenye michezo yao ya kirafiki waliyoicheza ikiwa ni maandalizi kuelekea msimu huo.

"Kwa sasa ninaendelea kujenga kikosi changu ili msimu utakapoanza tuweze kutimiza malengo tuliyojiwekea na ninaomba mashabiki wetu waendelee kutupa ushirikiano," alisema Kocha huyo.

Aliongeza kuwa mpaka sasa tayari amemaliza kufanya usajili wa wachezaji na kuahidi kuwatangaza ifikapo Agosti 10 mwaka huu katika tamasha lao.

Hadi sasa timu tayari Mashujaa imecheza michezo mitatu ya kirafiki ambapo mchezo wa kwanza alicheza na Marimbo FC (kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) na kulifungwa mabao 3-0, mchezo wa pili walicheza na Prisons na wakafungwa 1-0, huku pia wakicheza na KMC ambapo walitapata ushindi wa 2-0.



Mchezaji wa mpira wa Tennis, Pendo James, akipiga mpira kurudisha kwa mchezaji mwenzake katika mazoezi yanayosimamiwa na Kocha Riziki Salum, wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya Kenya Open Championships mwezi huu, nchini humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Malindi yaunda kamati ya usajili

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

WAKONGWE wa soka visiwani Zanzibar, Malindi SC imeunda kamati maalum ya usajili ili kuifanyia maboresho timu hiyo.

Kamati hiyo ina jumla ya watu nane ikiwa na Mwenyekiti na katibu pamoja na wajumbe sita.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Habari wa timu hiyo, Nassir Seif alisema lengo la kuundwa kwa kamati hiyo ya usajili ni kuiboresha timu hiyo ambayo imekuwa haifanyi vizuri katika michezo ya ligi kuu ya Zanzibar.

Alisema uwepo wa kamati hiyo utaweza kutoa nafasi kwa wajumbe wake kutafuta wachezaji wazuri na wenye viwango vikubwa watakaoleta ushindani katika ligi kuu ya Zanzibar

Alisema kuwa uongozi wa timu hiyo unaamini kuwa iwapo kamati hiyo itaweza kufanya kazi yake vyema katika kusajili wa wachezaji wazuri watafanikiwa kuwa katika nafasi za juu katika ligi ya msimu huu.

Aidha alisema kamati hiyo tayari ishaanza kazi yake ya kutafuta wachezaji ambao wataungana na timu hiyo katika safari yao ya msimu mpya wa Ligi.

Akiwataja wajumbe wa kamati hiyo ni Mwenyekiti, Mohmed Ali Jabri na Katibu wake ni Mohmed Massoud.

Kwa upande wa wajumbe ni Jafar Hassan 'Jef', Hassan Silima, Halibu, Mohmed Ali pamoja na Makocha wawili wa timu hiyo ambao ni Abdulghan Himid Msoma na Suleiman Mohmed 'Mo'.

# NAMUNGO YASHUSHA KIUNGO MKONGOMANI

Na Adam Fungamwango

KATIKA kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Namungo imeonekana kucharuka kuelekea mwishoni mwa dirisha kubwa la usajili kwa kushusha vifaa mfululizo, ambapo imefanikiwa kupata saini ya kiungo mshambuliaji wa FC Robi, Ritchi Nkoli.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana, inasema kuwa mchezaji huyo ni baadhi ya wachezaji ambao inaamini wataifanya timu hiyo kuwa imara na kufanya vyema kwenye Ligi Kuu Tanzania bara.

"Tunayo furaha kumtambulisha kiungo mshambuliaji kutoka DR Congo, Nkoli (Ritchi) kama mwanafamilia katika kikosi chatu cha Namungo," ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Mbali na mchezaji hiyo, klabu hiyo pia imetangaza kumsajili beki wa kushoto kutoka Geita Gold, Antony Mligo katika harakati zile zile za kuimarisha kikosi chao.

Mligo ni mmoja wa wachezaji ambao wamebaki Ligi Kuu, licha ya timu yao kushuka daraja, akiwemo Mashaka Velantino ambaye amesajiliwa na klabu ya Simba.

Ukiachana na wachezaji hao, Namungo imewasajili pia kina Lenny Kisu, Erick Molongi, Rafael Daudi, Djuma Shaaban, Beno Kakolanya. Msimu uliopita, ilimaliza nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikikusanya pointi 36 kwa michezo 30 ambazo imecheza, ikishinda nane, sare 12, na kupoteza michezo 10.

Tayari imeshacheza mechi moja ya kirafiki wiki hii dhidi ya Dodoma Jiji na kukubaki kipigo cha mabao 3-0, katika mechi iliyochezwa, Uwanja wa Black Rhino, Karatu, Arusha.

## ZISIKUPITE

### SACHO AWINDWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain ina makubaliano ya awali na mshambuliaji wa England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 24, lakini lazima wafikie bei inayotakiwa na Manchester United ya takribani pauni milioni 50. ***(Sports Zone)***

### NYOTA WAWANIWA MAN

MANCHESTER United inaweza kumgeukia beki wa kulia wa Ufaransa, Nordi Mukiele mwenye umri wa miaka 26, na kiungo wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte au mlinzi wa kati wa Slovakia Milan Skriniar mwenye miaka 29. ***(Express)***

### W'HAM YAMTAKA BISSAKA

KLABU ya West Ham imeanzisha mazungumzo juu ya mkataba wa beki wa kulia wa England, Aaron Wan-Bissaka kutoka Manchester United, ambaye thamani yake ni ya zaidi ya pauni milioni 15. ***(Sky Sports)***

### CHIESA ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA imefanya mawasiliano na mshambuliaji wa Juventus na Italia, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 26 ambaye pia anasakwa na Tottenham Hotspur. ***(Team talk)***

### GENOA MACHO KWA DE GEA

KLABU ya Genoa bado inashinikiza kupata mkataba na mlinda lango wa zamani wa Hispania, David de Gea mwenye umri wa miaka 33 ambaye hajacheza tangu aondoke Manchester United Julai 2023. ***(Football Italia)***

### PHILLIPS KUTIMKIA ASTON VILLA

KLABU ya Aston Villa imewasilisha ofa ya mkopo kwa kiungo wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28. ***(Football Insider)***

### O'BRIEN ATAKIWA EVERTON

KLABU ya Everton imekubali mkataba wa takribani pauni milioni 22 kumsaini beki wa Jamhuri ya Ireland, Jake O'Brien mwenye umri wa miaka 23, kutoka klabu ya Ufaransa ya Lyon. ***(Sky Sports)***

### RAK-SAKYI HAITAKI S'HAMPTON

WINGA wa Crystal Palace, Jesurun Rak-Sakyi mwenye umri wa miaka 21, anapendelea kuhamia Southampton kuliko Leeds msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### FOFANA KUTIMKIA ENGLAND

KLABU ya West Ham iko tayari kukidhi hitaji la bei ya AS Monaco la Euro milioni 35 kwa kiungo wa kati wa Ufaransa, Youssouf Fofana mwenye umri wa miaka 25. ***(L'Equipe)***


### ROYAL AKARIBIA MILAN

KLABU ya AC Milan inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili beki wa Brazil, Emerson Royal mwenye umri wa miaka 25 kutoka Tottenham Hotspur. ***(Fabrizio Romano)***

### GYOKERES KUTUA ARSENAL

ARSENAL ipo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres kutoka Sporting Lisbon, huku Liverpool ikiwa hawajajiandaa kuwasilisha ombi la kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Team talk)***

## DON SOKA MAG LAYA



# BAYERN MUNICH KUMBAKISHA SANE

**Licha ya tetesi za nyota huyo kutakiwa England na klabu ya Arsenal, bado klabu yake ya sasa ina....**

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich ina matumaini ya kumbakisha winga Leroy Sane kuelekea msimu mpya wa Bundesliga, huku kukiwa na ripoti za mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani kutakiwa Arsenal.

Sane ameingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake huko Allianz Arena, na hivyo kuzua maswali ya wazi kuhusu mustakabali wake, na ripoti nchini Ujerumani zinadai Arsenal wanatazamia kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kwa bei iliyopunguzwa.

Licha ya hali ya mkataba wake, vyanzo vimethibitisha kwamba Bayern hawana haraka ya kuachana na Sane na wanatarajia kusalia naye kwa angalau miezi 12 na uwezekano wa kuongeza mkataba wake.

Arsenal wanajulikana kuwa wapenzi wa Sane lakini bado hawajasonga mbele zaidi ya hatua hiyo na kwa sasa wanaelekeza nguvu zao kwa walengwa wengine, ambao ni kiungo wa Real Sociedad, Mikel Merino.

Iwapo Arsenal itatafuta winga mpya msimu huu wa joto, inatarajiwa kutafuta chaguo la kikosi ambacho labda hakitapata nafasi ya kuanzia mara moja.

Sane anatafuta muda wa kucheza zaidi na atafikisha miaka 29 Januari, na hilo linaweza kuwashawishi Arsenal kutafuta kwingine.

Kimsingi winga wa kulia, uhamisho wowote kwenda Arsenal utahitaji Sane kukubali jukumu la ziada.

# REAL MADRID HAITASAJILI TENA MSIMU HUU

**MADRID,** HISPANIA



KOCHA mkuu wa Real Madrid, Carlo Ancelloti amethibitisha kwamba klabu hiyo haitafanya usajili tena wala kuuza mchezaji yoyote na sasa inajiandaa na msimu mpya wa LaLiga na michuano ya Ulaya.

Licha ya kufanya usajili mkubwa wa Kylian Mbappe na Endrick, tetesi nyingi zimekuwa zikieleza kwamba klabu hiyo ilikuwa sokoni kutafuta mlinzi wa kati lakini sasa ipo wazi klabu hiyo haitafanya hivyo baada ya kauli hii kutoka kwa Don Carlo.

Baada ya kuondoka Nacho Fernandez na Rafa Marin, Real Madrid imebaki na wachezaji watatu tu ambao hawana majeraha, wachezaji hao ni Antonio Rudiger, Eder Militao na Jesus Vallejo.

David Alaba ni mlinzi mwingine lakini yeye bado hajapona majeraha ya goti mpaka mwisho wa mwaka au mwanzoni mwa mwaka 2025.

"Kikosi kimesharudi. Vallejo amerejea, Alaba anaendelea kupona na tuna vijana kama Joan, Jacobo na Raul (Asencio ). Hakuna atakayeondoka kwa sababu kila mmoja anataki kubaki," alisema Ancelloti.

# Rashford aongeza majeruhi Man Utd

**SAN DIEGO,** MAREKANI



KLABU ya Manchester United inakabiliwa na matatizo zaidi ya majeraha baada ya Marcus Rashford kulazimishwa kutolewa nje wakati wa mechi yao ya kirafiki dhidi ya Real Betis juzi.

Rashford alifunga penalti ya kipindi cha kwanza katika ushindi wa mabao 3-2 kwa United kwenye Uwanja wa Snapdragon lakini nafasi yake ikachukuliwa kipindi cha pili baada ya kuumia kifundo cha mguu wake wa kulia.

Mshambuliaji huyo wa England alihitaji matibabu uwanjani na alikuwa akichechemea alipokuwa akiondoka uwanjani.

Antony pia alitoka nje baada ya kudumu kwa dakika 23 tu kufuatia kutambulishwa kwake kama mchezaji wa akiba wa kipindi cha pili.

Matatizo zaidi ya majeruhi ni jambo linalomtatiza kocha, Erik ten Hag kwani ameshawapoteza Leny Yoro na Rasmus Hojlund.

Yoro atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa miezi mitatu kutokana na jeraha la mguu huku Hojlund atakosekana kwa wiki sita kutokana na tatizo la misuli ya paja.

Majeraha kwa wote wawili Hojlund na Rashford yangemwacha Ten Hag na mchezaji mpya aliyesajiliwa Joshua Zirkzee kama mshambuliaji wake pekee wa kati anayetambulika mwanzoni mwa msimu wa Ligi Kuu, ambao utaanza dhidi ya Fulham huko Old Trafford Agosti 16.

Zirkzee hayumo katika kikosi kwa ajili ya ziara ya Marekani baada ya kushiriki michuano ya Ulaya lakini amerejea mazoezini Carrington.

# Chelsea wakubali kumuuza Gallagher

**LONDON,** ENGLAND

CHELSEA imekubali dau la pauni milioni 33 kabla ya nyongeza kutoka kwa Atlético Madrid kwa Conor Gallagher baada ya kiungo huyo kukataa ofa ya mkataba mpya wa kubakia Stamford Bridge, kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 bado hajakubaliana na klabu hiyo ya LaLiga na ataamua hatma yake siku zijazo huku mazungumzo yakiendelea.

Gallagher amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake uliopo Stamford Bridge na The Blues wamedhamiria kutompoteza kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake utakapokamilika msimu ujao wa majira ya joto, kama ilivyokuwa kwa Andreas Christensen na Antonio Rüdiger, waliojiunga na Barcelona na Real Madrid.

Vyanzo vimesema pendekezo jipya la Chelsea kwa Gallagher lilikuwa mkataba wa miaka miwili na chaguo la msimu wa tatu na ulijumuisha nyongeza kubwa ya mshahara.

Hapo awali Gallagher alikataa kuhamia Aston Villa huku Tottenham Hotspur nao wakifuatilia hali yake kwa miezi kadhaa.

Pia vyanzo viliiambia ESPN kwamba Atlético Madrid iko kwenye mazungumzo na Villarreal juu ya uhamisho wa Alexander Sørloth baada ya dili la mshambuliaji wa Girona Artem Dovbyk kutokamilika.

Atlético inafahamika kuwa walikuwa na mpango wa Dovbyk kuchukua nafasi ya Álvaro Morata wiki iliyopita, lakini mazungumzo yalivunjika baada ya wakala wake kuongeza mahitaji yake ya kifedha dakika za mwisho.



HABARI MICHEZO

# EXTRA BONGO YASAKA MAKAZI YA KUDUMU

Na Sabato Kasika

BENDI ya muziki wa dansi ya Extra Bongo ambayo kwa miezi mitatu sasa iko mjini Songea mkoani Ruvuma, inatarajia kuhamishia maskani yake kati ya jiji la Dar es Salaam au Dodoma.

Mkurugenzi wa bendi hiyo, Ally Choki, aliliambia gazeti hili jana kwa njia ya simu kuwa, katikati ya mwezi huu, atakuwa ameshapata uhakika ni wapi Extra Bongo itahamia kati ya majiji hayo mawili.

"Unajua kwa sasa muziki ni popote, hivyo tutakaa tuamue ni wapi tuhamie, ingawa nguvu kubwa inaelekezwa Dodoma, kwani hatupendi kubanana na utitiri wa bendi Dar es Salaam," alisema Choki.

Alisema, kubanana na bendi nyingine Dar es Salaama ni kutafuta ugomvi, na kwamba wanadhani ni bora waweke maskani mkoa mwingine tofauti na jiji hilo.

"Hapa Songea bendi yetu imepata umaarufu mkubwa, haina mpinzani, lakini kwa sababu tulikuja huku kwa lengo moja la kuweka kambi, tunaona muda unatosha, sasa tunahamia kwingine," alisema.

Choki alifafanua kuwa kwa sasa bendi yake imeandaa nyimbo nyingi, na kwamba haina haraka ya kuzirekodi, badala yake itakuwa inaangusha mojamoja kadri inavyowezekana.

Alitaja baadhi ya nyimbo hizo kuwa ni ,Mpigakasia, Kinyago Changu, Jicho la Tatu na Penati ya Mwisho', ambao alisema umeipa umaarufu mkubwa bendi na kusababisha waache kurekodi nyimbo mpya kwa sasa.

"Kwa nyimbo hizi ambazo zinaendelea kutamba, hatuna haraka ya kuingia studio, bali tunaendelea kuzitangaza kwenye maonyesho yetu, hivyo katikati ya mwezi huu tutabisha hodi kati ta Dar na Dom," alisema.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kamunyonge, Manispaa ya Musoma mkoani Mara, wakiimba wimbo wakati wa mapokezi ya Mwenge wa Uhuru uliofika shuleni hapo juzi, kuzindua klabu ya mazingira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ufudu aanza kwa mkwara Mashujaa

Na Adam Fungamwango

KIUNGO mshambuliaji mpya wa Mashujaa FC, Ally Nassor ,Ufundu' ameanza kazi kwa kishindo katika timu hiyo, baada ya kupachika mabao yote mawili katika mechi ya kirafiki dhidi ya KMC, iliyopigwa juzi Uwanja wa Manispaa Kinondoni, Dar es Salaam.

Ufudu aliyesajiliwa msimu huu akitokea Kagera Sugar, alikuwa shujaa katika mchezo huo wa kujipima nguvu kwa timu zote ambazo zinajiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajia kuanza kutimua vumbi, Agosti 16 mwaka huu.

KMC imekumbana na kipigo hicho siku chache tu baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 5-0 dhidi ya PCC Eagles Men's Soccer ya Marekani, inayomilikiwa na Chuo cha Michezo cha Taasisi moja ya Kidini, iliyopo Pensacola, Florida nchini humo.

Timu zote, Mashujaa na KMC zilicheza baadhi ya wachezaji wao wapya mabao imewasajili kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu.

Mashujaa inayonolewa na kocha Mohamed Abdallah ,Bares' imefanya usajili wa wachezaji Seif Karihe kutoka Mtibwa Sugar, Chrispin Ngushi wa Yanga, Abdulmalik Zacharia akitokea Namungo, Mohamed Mussa, straika wa zamani wa Simba, Carlos Protus, Mathew Michael, Ismail Mgunda, Robert Mathias, Ufudu na wengineo huku KMC ikiwasainisha Imasil Mpaki, Ajoh Austin, straika kutoka Cameroon, Oscar Paul, Nickson Kassam Mosha, akitokea kikosi cha vijana cha Mtibwa Sugar, kipa raia wa Burundi aliyekuwa akiidakia klabu ya Vipers ya Uganda, Fabien Mutombora, Jean Nyezimana kutoka, Vital'O ya Burundi na beki wa kati Salum Athumani ,Stopper' kutoka KVZ ya Zanzibar.

## Aziz Ki aweka rekodi Sauzi, Yanga waitwa

INATOKA UK. 24

Naye winga wa timu hiyo, ambaye alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo msimu uliopita akitokea Prisons, Edwin Balua, alisema kambi yao ilikuwa nzuri na kila kitu kimekwenda kama kilivyopangwa, hivyo kitendo cha mashabiki kumaliza tiketi zote kinaonesha kuwa wana imani nao.

"Maandalizi yalienda vizuri sana, vitu vizuri tumevifanya inavyotakiwa, Wanasimba wajiandae kupata vitu vizuri," alisema mchezaji huyo.

Naye meneja aliyerejea tena kwenye timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema wamemaliza awamu kubwa ya maandalizi kilichobaki ni mambo madogo tu, lakini akiwa na imani kubwa ya kufanya vyema msimu huu.

"Tumemaliza awamu yetu kubwa, kwa maana ya msimu mpya kuelekea 2024/25, tumejiandaa vizuri na tuna imani tutafanya vizuri kwa msimu huu,"alisema.

Wakati huo huo, wasanii maarufu kutoka Arusha, Wadudu, wametoa wimbo watakaoutumia kwenye tamasha la Simba Day, uitwao ,Ubaya Ubwela', neno ambalo ndiyo kauli mbiu ya klabu hiyo kwa msimu huu.

Wadudu ni moja kati ya wasanii waliopewa fursa ya kutumbuiza kesho, kwenye tamasha la 16 la klabu hiyo tangu lianzishwe.

Kabla ya mchezo husika kutakuwa na burudani mbalimbali kutoka kwa wasanii wengi mashuhuri nchini, kabla ya utambulisho wa wachezaji wote wa zamani na wapya, ambao watatumika kwa msimu ujao wa mashindano.

Wachezaji wapya wa Simba wanaotarajiwa kutambulishwa ni Jushua Mutale, Steven Mukwala, Jean Charles Ahoa, Debora Fernandes Mavambo, Augustine Okajepha, Valentin Nouma na Karaboue Chamou, ambapo wazawa ni, Abdulrazack Hamza, Valentino Mashaka, Omari Omari, Kelvin Kijili na Yusuph Kagoma.

Simba ilifanya tamasha lake la kwanza Agosti 8, mwaka 2009, ambapo ilicheza na SC Villa ya Uganda kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru) na kushinda bao 1-0 lililowekwa wavuni na Hirally Echessa na baada ya hapo kila mwaka limekuwa linafanyika hadi leo.

## Harmonize, Marioo, Bella kunogesha

INATOKA UK. 24

uwanja," alisema Bella.

Naye Harmonize alisema anaamini mashabiki watajitokeza kwa wingi uwanjani kutokana na wasanii watakaokuwepo.

"Nipo tayari kuwapa burudani mashabiki wa Yanga siku hiyo nikiambatana na madansa wangu nitaonyesha shoo ya aina yake," alisema Harmonize.

Michezo
Nipashe Ijumaa Agosti 2, 2024

**Bayern Munich kumbakisha Sane**
UKURASA 21






Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa Benki ya CRDB na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa akisaini jezi rasmi ya CRDB Bank Marathon msimu wa tano jana muda mfupi baada ya uzinduzi ulioenda sambamba na kutangazwa kwa zawadi za washindi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachezaji Simba watoa ahadi nzito

●●●Wataka mashabiki kesho kwenda kwa wingi kwa Mkapa, wakashuhudie walichokifanya Misri...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kikosi cha Simba kuwasili juzi kutoka nchini Misri kilipokuwa kwenye kambi ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano, wachezaji wamewashukuru wanachama na mashabiki kwa kumaliza mapema kukata tiketi za kilele cha tamasha la Simba Day kesho, huku wakiahidi kuwalipa kwa kandanda safi la uhakika na ushindi si katika mechi hiyo dhidi ya APR ya Rwanda, bali msimu mzima wa mashindano.

Nahodha wa timu hiyo, Mohamed Hussein ,Tshabalala', amesema kitendo cha wanachama na mashabiki kumaliza tiketi 60,000 za tamasha hilo litakalofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kimewapa nguvu wao kama wachezaji na kimewafanya wawe na kazi ya kufanya ili kuwaburudisha na kuwafurashisha kwa soka safi pamoja na ushindi uwanjani.

"Kwa ujumla sisi kama wachezaji imetupa morali sana kuwa mashabiki wetu wanatufuatilia, wanatupenda na wapo karibu na sisi kwa vipindi vyote. Kwa ujumla tumefanya maandalizi mazuri sana, tunawaita wanachama na mashabiki wa Simba wenye tiketi zao mkononi waje waione timu yao, waangalie ni kitu gani ambacho tumekifanya nchini Misri, naamini msimu huu utakuwa ni bora sana kwetu,“ alisema nahodha huyo.

Tshabalala hakutaka kabisa kuuzungumzia mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga, akisema kwa sasa akili yao watu wote, viongozi, makocha na wachezaji ni katika tamasha la Simba Day tu na si vinginevyo.

"Kwanza tuna mchezo Jumamosi wa Simba Day dhidi ya APR ya Rwanda, mechi ya tarehe nane tutaizungumzia baada ya tamasha letu kupita,“ alisema.

INAENDELEA UK. 23

# Harmonize, Marioo, Bella kunogesha kilele cha Wananchi

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA kilele cha wiki ya Mwananchi kitakachofanyika keshokutwa Jumapili kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, uongozi wa Klabu ya Yanga umetambulisha wasanii watakaotoa burudani siku hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Makao makuu ya Klabu hiyo yaliyopo mtaa wa Jangwani, Msemaji wa Yanga, Haji Manara aliwataja wasanii hao kuwa ni msanii wa muziki wa bongofleva Rajab Abdul maarufu kama Harmonize, Omari Mwanga (Marioo) msanii wa muziki wa dansi Christian Bella pamoja na wengineo.

"Leo (jana) ni siku muhimu ya kutambulisha wasanii ambao watatumbuiza siku ya kilele cha wiki ya Mwananchi ni wasanii ambao wana uwezo mkubwa wanapokuwa jukwaani tunaomba mashabiki waje kwa wingi siku hiyo," alisema Manara.

Manara aliwataka mashabiki wao waendelee kununua tiketi kwa ajili ya kuingia uwanjani kuangalia wachezaji wao wapya waliosajiliwa msimu huu pamoja na kuangalia mchezo wa kirafiki kati yao na timu ya Red Arrows ya Zambia.

Alisema hawafanyi biashara ya ulanguzi bali wanauza tiketi kwa kufuata sheria na taratibu zinazohitajika na kudai siku hiyo hakutakuwa na tiketi zitakazouzwa nje ya uwanja.

Kwa upande wake mwanamuziki Bella alisema amejipanga vizuri kuwapa burudani mashabiki siku hiyo na kuwataka waje kwa wingi uwanjani.

"Kwa upande wangu nimejipanga vizuri kutoa burudani siku hiyo ninaomba mashabiki tuendelee kununua tiketi ili tuje tujaze

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042